Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 75 No. 185 | RABIUL2-JUMAD2 1437 AH | FEBR./MACHI 2016 | TAB./AMN. 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Bila shaka katika matukio yao ya kihistoria mna onyo kubwa kwa wenye akili. Si maneno yaliyozushwa, bali ni hakikisho la yale yaliyopo mbele yake, na ni maelezo ya kila kitu, na ni mwongozo na rehema kwa watu wenye kuamini.
(*12:112*)

Hakuna mafundisho yanayoweza kuishinda Islam

Allah Ameahidi ulinzi Wake

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Katika hotuba ya sala ya Ijumaa ya tarehe 11, Disemba 2015, Hadhrat Khalifatul Masih (Kiongozi wa Jamaat Ahmadiyya duniani), Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alizungumzia juu ya uzuri wa mafundisho ya Islam sambamba na ahadi ya ulinzi kutoka kwa Allah.

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Khalifa mtukufu a.t.b.a. alisema:

Hivi karibuni mwandishi mmoja wa gazeti aliandika, na pia mwanasiasa mmoja wa Australia alisema kuwa Waislamu kuwa magaidi ni kwa sababu ya mafundisho ya Kiislamu ya Jihad na amri nyingine za Uislamu. Mwanasiasa mmoja mtumishi wa Serikali hapa nchini Uingereza pia alisema kuwa kuna baadhi ya amri nyingine katika Uislamu ambazo zinaelekeza watu kwenye siasa kali.



Baitul Islam Mosque, Maple Ontario Canada

ISIS waliteka maeneo ya Iraq na Syria na kujiundia mamlaka yao wenyewe. Wao wanaiogofya dunia ya Magharibi kwa mtindo wao wa kushambulia kwa njia za kikatili na kuua watu wasio na hatia. Hali hii inawatia watu hofu sana na imewapa nafasi ya kuushambulia Uislam wale baadhi ya viongozi ambao hawana uelewa wa mafundisho ya Islam, au wale ambao siku

Endelea uk. 3

Kutimia kwa bishara ya Musleh Mauud

Kunathibitisha ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. katika hotuba yake ya Ijumaa ya tarehe 19/2/2016 alizungumzia juu ya kutimia kwa bishara ya Musleh Mauud na kueleza kwamba jambo hilo linahibitisha ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Baada ya Salamu, Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, Khalifa mtukufu a.t.b.a. alisema:

Tarehe 20 Februari inatambulika kuwa ni siku ya kutangazwa kwa bishara ya Musleh Maud ndani ya Jamaat Ahmadiyya. Katika bishara hii Mwenyezi Mungu alimfahamisha Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba atampatia mwana ambaye atakuja kuihudumia imani, mwana ambaye atakuwa na sifa nyingi. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kwamba hii haikuwa bishara ya kawaida tu bali ilikuwa ni bishara kuu ya kimbingu ambayo Mwenyezi Mungu Ameionyesha kwa ajili ya ukweli na adhama ya mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Na ishara hii ni bora zaidi, na iliyo kuu na yenye utukufu kuliko ishara ya kumfufua mfu na kumrudishia uhai. Ukweli ni kwamba roho ya mtu aliyekufa inaweza tu kurudishwa duniani kupitia maombi na jambo hili bila shaka ni lenye kubishaniwa. Ingawaje katika bishara hii kwa fadhili za Mwenyezi Mungu na baraka za mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema, maombi yake yamekubaliwa na ahadi imewekwa ya kumtuma Roho aliyebarikiwa ambaye kudhihiri kwake na sifa zake tukufu zitaenea duniani kote. Hata kama bishara hii ionekane kufanana na bishara ya kumfufua mfu lakini baada ya kutafakari itadhihirika kwamba hii ni bishara bora mara mamia zaidi kuliko kumfufua mfu. Roho ya mfu hurudishwa duniani kwa njia ya maombi lakini hapa nafsi ilitumwa kwa njia ya maombi, lakini roho zile na roho hii zimetofautiana sana kama zilivyotofautiana pembe mbili za dunia.



Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, Musleh Mauud, Khalifatul Masih II r.a.

Kwa hakika, dunia ilishuhudia kwamba bishara hii ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) ilitimia kwa utukufu mkubwa. Na zama zimethibitisha kuwa aliyekuwa dhihirisho la ubashiri huu si mwingine ila Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmood Ahmad. Wanajumuiya waliona wakati huo ubashiri ulimhusu yeye lakini yeye mwenyewe hakusema lolote wala hakutangaza. Kiasi hiki kwamba miaka thelathini ya Ukhalifa wake ilipita. Hatimaye, alitangaza mnamo mwaka 1944 kwamba yeye kweli alikuwa ndiye Musleh Maud.

Mnamo Januari 28, 1944 Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema kwamba alitaka kusema kitu ambacho hakikumjia kama kitu cha kawaida kwake na ambacho yeye alikuwa na uzito na wasiwasi kukisema

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

DUNIA KIJIJI

Harakati za kuifanya dunia kuwa kijiji zilianzishwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliye ieleza dunia ya kwamba ina Muumba Mmoja na watu wote ni sawa na ubora wa mtu unatokana na Taqwa na wala sio rangi yake.

Ni jambo la kusikitisha sana, kwamba wasomi tulio nao hivi leo duniani hawajachukua taklith ya kumuelewa, kumsoma na kutafiti maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Kwa mathalani wasomi wengi wa nchi za Ulaya na Marekani wana itikadi kwamba katu Waislam hawawezi kuwa raia wema na watiifu katika nchi ambazo hazikusimama kwenye mafundisho ya Islam. Na hivyo wasomi hao wanaendelea kujenga hoja yao muflisi kuwa Waislam ni tishio kwa maendeleo na amani duniani.

Hoja hizo zingejengwa na akina yakhe! Weka mchuzi pangu pakavu, tungeweza kuelewa na kuvumilia. Lakini masikitiko yetu makubwa yamezidi tunapoona hoja hizi zimetolewa na watu waliopata bahati ya elimu, bahati ya kusoma historia. Nani asiyejua kwamba Waislam walipoteswa katika mji wa Makka walilazimika kuishi Uhabeshi na huko Uhabeshi walipokelewa na kupewa hifadhi na kuishi huko kwa salama na amani. Kutokana na mafundisho mazuri ya dini tukufu ya Islam, Waislam wanaweza kuishi mahali popote tena kwa heshima na taadhima. Fundisho la msingi la dini tukufu ya Islam kama lilivyofafanuliwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kuipenda nchi ni sehemu ya imani. Kuipenda nchi, kuitetea na kuilinda. Hayo yote katika Islam si mambo ya hiyari, ni wajibu wa kila Muislam. Na kumbuka basi kwamba neno lolote linalotolewa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa hakika ni neno la Mwenyezi Mungu. Kumbuka pale alipotupa changarawe na ikasemwa kwamba aliyetupua ni Allah. Hivyo Muislam ana uwezo na amefundisha ya kwamba anaweza kuishi mahali popote.

Itikadi ya Waislam ya kwamba tunao wajibu wa kuheshimu Manabii wote, inajenga mapenzi na kuheshimiana. Mawaidha yetu ya dini yanakwenda kwa njia ya heshima na busara. Tumefundisha kujenga hoja na hoja zenye mashiko. Si kwa nguvu bali nguvu ya hoja ndiyo inayotawala.

Mambo yafuatayo yanazidi kujenga hoja ya kwamba Muislam anayeielewa dini yake vizuri hana tatizo lolote la kuishi mahali popote duniani. Kwani ni dhahiri ya kwamba hakuna mgongano wa kimaslahi kati ya kuipenda Islam na kuipenda nchi. Muislam siku zote amefundishwa asisaidie katika ukatili na ukandamizaji. Hivyo atafanya kila jitihada ya kwamba ukatili umeondoka katika ardhi. Na pia mafundisho ya Islam yanazidi kumuelekeza ya kwamba mikono yake na ulimi wake vyote hivyo viwe salama kwa watu wengine. Mtu wa namna hii atashindwaje kuishi mahali popote?

Muislam pia ameambiwa ya kwamba popote alipo akikipata kitu chochote kilicho kizuri. Aelewe kwamba hicho kitu ni mali yake na anapaswa kukichukua. Mtu kama anaishi katika jamii fulani na akafuata mafundisho hayo atakosaje kuishi kwa salama na amani? Muislam pia anasisitizwa ya kwamba ana wajibu wa kuamrisha mema na kukataza mabaya. Masikini anapewa haki zake na Muislam pia ni mtu ambaye anatimiza ahadi na mapatano.

Mafundisho yote haya kama yanafuatwa vizuri na yanatekelezwa kwa uadilifu yanampa fursa Muislam kuishi mahala popote pale. Hivyo wasomi wa Ulaya na Marekani ambao wanafikiri ya kwamba Muislam hawezi kuishi katika utamaduni wa Magharibi wanakosea sana. Islam ni dini ya njia ya kati, na aendaye njia ya kati hufika salama.

Kutimia kwa bishara ya Musleh Mauud

Kutoka uk. 1

lakini kwa vile jambo hilo limeshikamana na mipango ya Mungu kama vile ulivyo Utume, yeye hakuwa na chaguo isipokuwa kusema kuhusu jambo hilo. Yeye akaeleza kuhusiana na ndoto yake ndefu aliyoipata na kusema kwamba Mungu Alikuwa amekadiria kupitia dhati yake kutimizwa kwa bishara ya Musleh Maud. Alisema watu walikuwa wakirudia rudia kuuliza maoni yake juu ya bishara hiyo lakini hajawahi bali hata hajajaribu kuisoma bishara hiyo kwa kina ili asije akapata mawazo ya kujidanganya.

Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema kuwa wakati fulani Hadhrat Khalifatul Masih I (r.a.) alimpatia barua ambayo iliandikwa na Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) kuhusu kuzaliwa kwa Hadhrat Musleh Maud na Hadhrat Khalifatul Masih I alimuagiza Hadhrat Musleh Maud kuichapisha kwenye jarida la Tasheezul Azhan. Kutokana na heshima na staha aliyokuwa nayo kwa Hadhrat Khalifatul Masih I, aliichapisha lakini hata hakuisoma mada iliyokuwemo ndani yake kwa umakini wakati huo. Wakati watu walipoeleza maoni yao juu ya kutimia kwa bishara hii katika dhati yake alikuwa akinyamaza kimya na bila kujibu. Alijisikia haikuwa muhimu kwa mtu ambaye ahadi hii ilitimia kwake kutangaza kwamba yeye alikuwa ndio dhihirisho la bishara hiyo. Kama vile Mtukufu Mtume (s.a.w.) alivyokuwa ametabiri kuhusu kutokea kwa treni na baada ya kutimia kwa bishara hiyo haikuwa lazima kwa treni kujitangaza. Wakati watu waliposisitiza kwamba kulikuwa na haja ya kujitangaza kuwa yeye alikuwa ndio dhihirisho la bishara hii alisema bishara yenyewe itajitimiliza kwa uwazi kwa watu kuona na kama bishara hii ilikuwa itimizwe katika dhati yake dunia itajionea yenyewe na kama ilikuwa isitimizwe katika dhati yake, pia dunia bila shaka itaona. Alisema hakukuwa na haja ya yeye kusema chochote kwa njia moja au nyingine.

Baadhi ya maneno ya ufunuo yalikuwa: 'Walisema kuwa yule asubiriwaye kwa hakika ni huyu au tumtazamie mwingine!' Watu kwa kurudia rudia walimuuliza Hadhrat Musleh Maud kuhusu bishara hii kwa kipindi cha muda mrefu. Kipindi hiki cha muda mrefu pia kilidokezwa katika bishara za Masihi Aliyeahidiwa (a.s.). Kama ilivyotajwa kumhusu Hadhrat Yaqub (a.s.) kwamba [watoto wake] ndugu wa Hadhrat Yusuf (a.s.) walikuwa wakimwambia kwa muda gani ataendelea kuzungumza juu ya Yusuf. Ufunuo huu pia alipewa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.), pia alipata na ufunuo huu: 'Mimi nahisi harufu ya Yusuf'. Hii ilikuwa ni kumtaarifu kwamba kutimizwa kwa bishara ya Musleh Maud kutadhihirika baada ya kipindi cha muda mrefu. Hadhrat Musleh Maud alikuwa na mawazo kwamba hata kama bishara hii haikujulishwa mpaka wakati wa kifo chake, hata hivyo mazingira na matukio yangebainisha kuwa bishara hiyo ilitimia katika dhati yake. Hata hivyo, alisema, Mwenyezi Mungu Alimjulisha kwamba yeye kwa hakika alikuwa ndiye dhihirisho la bishara ya Musleh Maud.

Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alitaja baadhi ya mambo kuhusu bishara ya Musleh Maud, kwa mfano, 'Yeye atabadilisha tatu kuwa nne' na 'Ni Jumatatu, Jumatatu iliyobarikiwa'. Inaulizwa, bishara hizi mbili zinamaanisha nini?.

Kwa upande wa: 'Atabadilisha tatu kuwa nne ' Hadhrat Musleh Maud alieleza kwamba yeye alikuwa mwana wa nne kuzaliwa kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.). Kabla yake, Mirza Sultan Ahmad, Mirza Fazl Ahmad na Bashir wa kwanza walizaliwa naye alikuwa wa nne. Hadhrat Musleh Maud alielekezwa na Allah kutafakari kwamba bishara haikutaja watoto wa kiume. Alisema alijisikia 'kubadilisha tatu kuwa nne' ilihusiana na zama za kuzaliwa kwake. Yeye alizaliwa katika mwaka wa nne baada ya ubashiri huu kutolewa. Bishara hii ilitolewa mwaka 1886 na Hadhrat Musleh Maud alizaliwa mwaka 1889. Miaka minne baada ya bishara, na kwa miaka mitatu iliyotangulia, hivyo kuigeuza mitatu kuwa minne.

'Ni Jumatatu, Jumatatu yenye baraka, inaweza kuwa na maana nyingine na umuhimu lakini Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alihisi kwamba Jumatatu ni siku ya tatu ya wiki na katika harakati za kiroho Manabii wa Mungu na Makhalifa wao wana zama zao. Wakati wa Mtume ni zama yenye haki yake yenyewe, kama wakati wa Khalifa ulivyo ni zama yenye haki yake yenyewe. Katika zama zetu hizi kipindi cha kwanza kilikuwa ni cha Masihi Aliyeahidiwa (a.s.), kipindi cha pili kilikuwa cha Hadhrat Khalifatul Masih I (r.a.) wakati kipindi cha tatu kilikuwa ni kile cha Hadhrat Musleh Maud.

Ufunuo mwingine wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) 'Fazl e Umer' [jina ambalo alipewa, kabla ya hajazaliwa] linawiana na hili. Hadhrat Umer (r.a.) alikuwa Khalifa wa tatu baada ya Mtume (s.a.w.). Hivyo, 'ni Jumatatu, Jumatatu yenye baraka haimaanishi siku yoyote maalum au siku yoyote yenye baraka maalum, badala yake, maana yake ni kwamba yeye atakuwa wa tatu miongoni mwa watu ambao watainuliwa ili kutumikia imani katika zama hizi. Hadhrat Musleh Maud r.a. alisema kuwa ufunuo huu pia unatimia katika dhati yake kwa namna ambayo ilikuwa nje ya uwezo wake. Alianzisha mpango wa Tehrik e Jadid mwaka 1934 katika kukabiliana na hali ambayo kwa vyovyote haikuwa kwenye mamlaka yake. Kutokana na mipango ya Serikali ya siku hizo kuchukua hatua kali dhidi ya Jama'at na hila mbovu za mwendeleo wa kundi la Ahrar, Mwenyezi Mungu aliuelekeza moyo wake kuanzisha mpango wa Tehrik e Jadid mwaka 1934 na alipanga awamu yake ya kwanza imalizike baada ya miaka kumi. Alisema baada ya kila kafara / muhanga kuna muda kwa ajili ya Eid. Hivyo mwishoni mwa awamu ya miaka kumi ya Tehrik e Jadid ilikuwa ni mwaka wa furaha na mwaka huo ulikuwa uanzie siku ya Jumatatu. Hivyo, yeye alieleza kuwa Mungu alitutaarifa kwa njia ya maneno haya kwamba wakati Islam itakuwa katika hali dhaifu, mpango imara kwa ajili ya uenezi wake utaanzishwa. Na hitimisho lenye mafanikio la awamu yake ya kwanza litakuwa ni nyakati za baraka kwa Jumuiya.

Miongoni mwa maneno ya ufunuo kumhusu Musleh Maud yalikuwa maneno haya: 'Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya Baraka za Roho Mtakatifu'. Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema aliona katika ndoto kwamba yeye anazivunja vunja

Endelea uk. 5

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Hakuna mafundisho yanayoweza kuishinda Islam

Kutoka uk. 1

zote wako dhidi ya Islam. Pia inaandikwa siku hizi kwamba dini zingine ziliwahi kuwa na mafundisho makali kama haya lakini ama wafuasi wake wamewacha kuyafuata au wameyabadilisha ili yaendane na wakati tulionao.

Wanapendekeza kwamba Quran tukufu nayo inahitaji kufanyiwa marekebisho ili iendane na zama hizi. Hili linathibitisha kwamba watu hawa wanakiri kuwa mafundisho wanayoyafuata hayatoki kwa Mungu bali ni zao la fikra za kibinadamu. Hali hii ilikadiriwa kutokea kwani hakukuwa na ahadi ya Kimbingu ya kulindwa kwa mafundisho haya hadi siku ya mwisho. Lakini Mwenyezi Mungu anasema kuihusu Quran tukufu kwamba:

Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao. (15:10).

Pia Mwenyezi Mungu amepanga mipango ya ulinzi wa Quran tukufu.

Katika maandishi yake kadhaa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ameifafanua aya hii kama ifuatavyo:

Imekuwa njia ya Mwenyezi Mungu, Mwenye Enzi tokea azali kwamba wakati anawakataza watu juu ya tendo fulani ni dhahiri kwamba katika hatima ya watu hao kuna baadhi miongoni mwao wataangukia kwenye kosa la kufanya kile walichokatazwa. Kama vile ambavyo aliwakataza Wayahudi katika Torati kwamba wasibadili maneno ya Mwenyezi Mungu basi hatimae baadhi yao waliyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Ingawaje Quran tukufu haisemi kwamba msibadili maneno ya Mwenyezi Mungu bali inasema: ***Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao.*** (15:10). (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II, p. 769).

Basi iwazi kutokana na aya hii kwamba wakati watu watakapoinuka kutaka kuuzima ukumbusho huu, Mwenyezi Mungu ataulinda kwa kumuinua mteule Wake kutoka mbinguni. (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II, p. 768)

Mara kwa mara watu hawa hupinga kuhusu mafundisho ya Qur'ani Tukufu na kujaribu kupindua maana yake kwa sababu mafundisho yao wenyewe aidha yameshapinduliwa kichwa chini miguu juu au yamebaki maandishi tu kwenye vitabu. Hivi karibuni ujumbe mfupi wa video ulikuwa ukisambazwa kwenye Whatsapp. Vijana wawili wa kiume walikuwa wakiwaonyesha watu vifungu fulani kutoka katika kitabu ambacho kwa jalada lake la juu walidai kuwa ni Qur'an. Wao walikuwa wakiwaonyesha watu mitaani na kila mtu aliyeviona vifungu hivyo alikubali kwamba yalikuwa ni mafundisho mabaya kabisa ya Uislamu ambayo yamesababisha Waislamu kuwa watu wenye msimamo mikali. Baada ya muda vijana hao waliondowa jalada la kitabu na ikabainika kwamba kwa hakika kitabu walichokuwa wakinukuu hakikuwa Qurani bali ni Biblia. Lakini baada ya hilo kubainika hakuna mtu yeyote, wanaume kwa wanawake, aliyekuwa akisema chochote kilicho hasi bali alicheka na kujiondokea. Mtu mmoja alisema ni jambo la kushangaza kwa sababu yeye tangu akiwa katika shule ya Kikristo alikuwa akisoma Biblia lakini hakuwahi kuwa na hata wazo kuhusu vifungu hivyo. Hii ndio hali yao; Kama Muislamu atafanya kitu kibaya wao mara moja watakihusisha na dini yake lakini kama mtu wa dini nyingine atafanya kitu kibaya yeye watamchukulia kuwa uwezo wake wa kiakili ni mdogo au ana matatizo ya kujifunza.

Tunakubali kwamba vitendo potofu vya baadhi vikundi vya Kiislamu vimeupa Uislamu jina baya kabisa. Hata hivyo, ni jambo ovu na lisilofaa kabisa kuyalaumu mafundisho ya Islam kwa kujificha nyuma ya mgongo wa matendo hayo maovu ya baadhi ya Waislamu, na kisha kuchupa mipaka kabisa juu ya lawama hizo. Moja ya kadhia iliyo dhidi ya Uislamu siku hizi inatoka kutoka kwa mmoja wa wagombea Urais wa Marekani. Kwa vyovyote wanaweza kusema wanavyotaka dhidi ya Islam, lakini hakuna dini yoyote wala hakuna sheria zozote zilizotengenezwa na watu na zikabatizwa jina la dini zinazoweza kushindana na Uislamu katika uzuri wa mafundisho yake.

Kwa mujibu wa ahadi ya Mungu mteule mmoja alitumwa katika zama hizi ili kulinda mafundisho ya Uislamu na kutufanya kufahamu uzuri wake. Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) anasema:

'Qur'ani ambayo pia hujulikana kama Dhikr (Onyo/Kumbuko) iliteremshwa katika siku za mwanzo kuwakumbusha kweli na sifa ambazo ni asili ya mwanadamu lakini walikuwa wamezisahau. Kwa mujibu wa ahadi kamilifu ya Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi (Arabic) '*...**hakika Sisi ndio Tuyalindao***' mwalimu alishuka kutoka mbinguni katika zama hizi pia. Yeye ni kielelezo cha:

'***Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao***; ... ' (62: 4) na kuja kwake kuliahidiwa. Naye ni yule ambaye sasa anaongea kati yenu. ' (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II, p. 770)

'Mwenyezi Mungu, Mwenye Adhama aliahidi' ***Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao.'*** na Akabeba wajibu wa kulinda Uislamu na Qur'ani Yeye Mwenyewe, ili kwamba apate kuwaokowa Waislamu na matatizo na kuwalinda dhidi ya kuanguka katika shimo la upotoshaji. Bahati njema ni ya wale ambao wanauthamini mwendeleo huu na kujipatia faida kutoka humo.' (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II, p. 770)

"Kwa mujibu wa ahadi yake '***Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao.'*** Mwenyezi Mungu, Mwenye amenituma mimi mwanzoni mwa karne ya kumi na nne ili nistawishe ukuu wa Qur'ani." (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II, p. 770)

'Hakuna kiongozi mwingine wa dini leo anayepata kusaidiwa na Mungu kwa namna ya msaada ambao upo pamoja nasi.' (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. II,)

Haya ni majibu ya pingamizi zinazotolewa dhidi ya Uislamu. Kukiri kwa watu wa dini nyingine kwamba wamebadilisha mafundisho yao ili yaendane na wakati ni uthibitisho kuwa dini zao si chochote zaidi ya kitu kilichokufa. Lakini maneno ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) kwa ulimwengu wa Kiislamu ni haya: Wanapaswa kuungana naye ili kuwanyamazisha wapinzani ambao wanadai Uislamu kuwa dini ya vurugu. Na wale wanaodai kueneza Uislamu kwa njia ya matumizi ya nguvu kwa hakika hao ni mikono tu au zana za wale wenye kupambana dhidi ya Uislamu. Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) amefafanua kwamba huu si wakati wa Jihad ya upanga. Ruhusa ya Jihadi ya Upanga ilikuwa tu iliyotolewa chini ya masharti maalum katika siku za mwanzoni mwa Uislamu wakati adui alitaka kuufutilia mbali Uislamu kwa kutumia upanga. Islam imejaa mafundisho ya upendo na amani na leo mafundisho haya yanahitaji kupandikizwa na kusambazwa. Kila Ahmadiya anahitaji kuelewa na kuyatekeleza mafundisho haya na kujitahidi kukuza uhusiano hai na Mwenyezi Mungu. Leo ni Ahmadiya pekee ambao wanaweza kutoa elimu hii kwa Waislamu na wasio Waislamu. Wale ambao wanaukosoa Uislamu ni wajinga nasi hatuna budi kuwajulisha juu ya ujinga wao/kutokujua kwao. Mafundisho ya Uislamu ni mafundisho ya amani na usalama na inabidi kutoa mafundisho haya katika mwanga wa Qur'ani tukufu. Tunatakiwa kuwauliza wengine wanawezaje kusema kwamba Uislamu ni dini ya vurugu wakati hawaujui? Pia Tuna wajibu wa kuwaambia Waislamu kwamba kwa kuuana wao kwa wao na kwa kuendekeza magomvi ya ubinafsi wa madhehebu kati yao wanauweka Uislamu katika hali mbaya kabisa.

Ingawaje uwezo wetu si mkubwa, bado tunapaswa kufanya kazi hii kwa kadri iwezekanavyo kupitia vyombo vya habari, njia za mawasiliano na njia nyingine katika kila nchi na kila mji. Ni muhimu sana kuujulisha ulimwengu juu ya picha halisi ya Uislamu. Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu Jumuiya yetu inazingatia hili karibu kila mahali lakini zama zinatuhitaji kwamba vyombo vya habari viendelee kutumika kwa kudumu kwa ajili hii. Mafungamano na vyombo vya habari lazima yaimarishwe na umma wapaswa kuwa na taarifa [ya mambo] kupitia vyombo vya habari. Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu tuna mahusiano mazuri na vyombo vya habari nchini Marekani na pia kuna baadhi ya mawasiliano hapa (Uingereza) na nchini Ujerumani. Lakini kuna haja kubwa ya kupanua mahusiano hayo.

Hivi karibuni mbunge Mwanamke kutoka Glasgow alizungumza katika Bunge la Uingereza kuhusu hali halisi ya Uislamu kwa mtazamo wa Jumuiya ya Ahmadiyya. Alisema Waislamu waahmadiyya wanatekeleza mafundisho ya Uislamu kwa vitendo. Alisema yeye amewahi kuhudhuria kongamano letu la amani huko Glasgow ambalo alilisifia sana. Mwanamama mmoja - Katibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ambaye pia alikuwa katika Baraza la Bunge alijibu kwa kusema kwamba Uislamu unaotekelezwa na Wanajumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni tofauti kabisa na Uislamu unaotekelezwa na wale wenye misimamo mikali. Aliongeza kuwa Waahmadia ni raia wa amani. Bila shaka ukweli ni kwamba Waahmadiyya hawawakilishi mafundisho yoyote mapya bali kwa hakika wanawakilisha mafundisho sahihi ya Qur'ani.

Hivyo, kama taarifa hii haifuatiliwi watu bila shaka watasahau haraka. Kauli nzuri kutuhusu sisi ilishawahi kutolewa pia katika Bunge la Uingereza lakini kisha ikasahaulika. Kinachotakiwa ni kuitunza hali hii katika akili za watu kwamba mafundisho ya Uislamu ni nini. Lakini baada ya kutajwa uzuri wetu usio wa kawaida katika vyombo vya habari, kisha ukimya hufuata. Mara mashambulizi ya kigaidi yanachukua nafasi na yanabeba vichwa vya habari vya magazeti na hapo tena fursa nyingine inapatikana kwa hisia zilizo kinyume na Islam kurushwa hewani.

Wakati wa ziara yake ya hivi karibuni ya nchini Japan watu wengi wakiwemo wasomi wenye elimu nzuri walizungumza na Hadhrat Khalifatul Masih. Kwa kweli Padri wa Kikristo alisema kuwa chochote Huzoor alichosema katika mwanga wa mafundisho ya Uislamu kinahitajika kuwafikia sio tu watu wa Japan bali dunia yote. Alisema kuwa ujumbe huo haupaswi kuishia kwenye tukio ambalo liliandaliwa tu bali unatakiwa ufikishwe kote nchini Japan kupitia juhudi zenye kuendelea. Sasa, watu waungwana nje Jumuiya pia wanatuambia kuwa haifai kwa sisi kukaa kimya bali wakati umefika tuyaweke mafundisho haya mbele ya dunia kwa kudumu, na kwamba ni kwa namna hiyo tu ndipo yatakapoweza kuwafaidisha wengine. Sasa ni kazi ya Jumuiya huko Japan kupanga na kuendeleza jambo hili kwa bidii kubwa. Vile vile, hapa nchini Uingereza na nchi nyingine za dunia ujumbe wa mafundisho mazuri ya Uislamu, ufahamu ambao sisi tumefanikiwa kuupata kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) ni lazima kusambazwa. Hakuna kinachoweza kushindana na mafundisho haya mazuri ambayo yanaelezewa kupitia mwanga wa Qur'ani tukufu.

Mwenyezi Mungu alimtuma Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) kuwasilisha tafsiri sahihi na ufafanuzi wa Qur'ani na hivyo kuulinda. Alitimiza kazi hii vizuri sana kupitia vitabu vyake, Malfudhaat na hotuba. Mungu alichukua jukumu la kulinda Qur'ani katika zama hizi kwa njia yake na pia ni jukumu la kila

Endelea uk. 4

Hakuna mafundisho yanayoweza kuishinda Islam

Kutoka uk. 3

Ahmadia kuubeba ujumbe huu na kuufikisha kwa watu wa kila tabaka katika jamii na kwa kila kundi lenye ushawishi.

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) aliandika kuhusu mafundisho ya amani ya Uislamu:

Ni dhahiri kwamba Islam haijawahi kushabikia matumizi ya nguvu / ulazimishaji. Iwapo Qur`an Tukufu, vitabu vya Hadithi na kumbukumbu za historia vitachunguzwa kwa uangalifu na pale inapowezekana iwapo vitasomwa au kusikilizwa kwa makini, itafahamika kwa yakini madai kwamba Islam ilitumia upanga ili kueneza Imani hiyo kwa nguvu ni madai ya aibu na yasiyokuwa na msingi dhidi ya Islam.

Dai kama hilo dhidi ya Islam linafanywa na watu ambao bado hawajaisoma Qur`an, Hadithi na taarikhi za kuaminika za Islam katika hali ya kujitegemea wao wenyewe, bali wameutegemea sana uwongo na kwa hiyo wakaleta madai yenye makosa dhidi ya Islam. Lakini najua kwamba wakati umeisha karibia ambapo wale wenye njaa na kiu ya kutafuta ukweli watatiwa nuru ya kujua iwapo kuna ukweli wowote katika madai haya. Je tunaweza kuielezea Imani hii kuwa ni imani ya kutumia nguvu wakati kitabu kitakatifu Qur`an, kinaelekeza wazi kwamba hakuna ushurutishaji katika mambo ya dini na kwamba hairuhusiwi kutumia shuruti au nguvu katika kumfanya mtu ajiunge na Islam? Je tunaweza kumshitaki Mtume yule Mkuu kwamba alitumia mabavu dhidi ya watu wengine, ambaye usiku na mchana kwa miaka kumi na mitatu aliwahimiza Masahaba zake wote mjini Makka wasirejeshe uovu waliotendewa na maadui, bali wavumilie na kusamehe? Lakini wakati fujo ya maadui ilipopita kiasi na wakati kila mtu alipokuwa anajitahidi kuufutilia mbali Uislam, Mwenyezi Mungu mwenye ghera Aliamua kwamba ulikuwa ni wakati muafaka wale watu waliopigana kwa upanga lazima wateketezwe kwa upanga. Waila Qur`an Tukufu haijaidhinisha kulazimisha. Kama kulazimisha kungeidhinishwa na Islam, Masahaba wa Mtume wetu Mtukufu (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) wasingeonyesha tabia ya watu wakweli na wanyoofu, wakati wa majaribu. Lakini utiifu na uaminifu wa masahaba wa Bwana wetu Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) ni jambo ambalo sina haja ya kulitaja. (Jesus in India, pp. 10-11)

Vita katika Islam ni vya aina tatu: (1) vita ya kujihami, yaani vita kwa sababu ya kujilinda; (2) vita ya kuadhibu, yaani damu kwa damu; (3) vita ya kupata uhuru, yaani vita ya kuvunja nguvu ya wale wanaowaua wale wanaojiunga na Islam. (Jesus in India, p. 11)

Quran Tukufu ina agiza wazi kabisa kuwa msinyanyue upanga kwa ajili ya kueneza dini bali mueleze sifa hasa ya dini na muwavutie watu kwa mifano bora. Na wala msidhani kwamba mwanzoni kulikuwepo na agizo la kunyanyua upanga ndani ya Islam, kwa sababu upanga huo haukunyanyuliwa kwa ajili ya kueneza dini bali kwa ajili ya kujihami na mashambulizi ya adui au ulinyanyuliwa kwa ajili ya kustawisha amani. (Nyota ya Kaisari, p. 11)

Wale wanaotambulika kama Waislamu lakini hawajui chochote katika Uislamu zaidi ya jambo hili kwamba Uislamu lazima uenezwe kwa nguvu hao hawana habari yoyote juu ya sifa nzuri na zilizo bora zilizomo ndani ya Uislam, na hivyo hali yao haitofautiani na ile ya wanyama pori. (Tafseer Hadhrat Masih e Maud, Vol. I, p. 747)

Basi Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) ametuhimiza kuuwasilisha mbele ya dunia uzuri wa asili wa Uislamu na kuongeza elimu yetu sisi wenyewe na kisha kuwavutia watu kupitia matendo mazuri. Kwa hakika ni jukumu kubwa juu ya kila Ahmadia kuongeza ujuzi wake wa Qur'an tukufu, kuwa mfano mzuri na kuivutia dunia. Ni kwa njia hii tu ndipo tutakapoweza, katika kuwa kwetu chini ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) kuutumikia Uislamu na Qur'ani Tukufu na kuijulisha dunia kuhusu hilo.

Qur'an inasema kuhusu wale wasiokubali ujumbe wake:

'***Na wakasema: Kama tukifuata mwongozo pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu.....***' (28:58).

Hapa mafundisho ya Uislamu hayakosolewi kwa misingi ya kuwa na vurugu.

Wale ambao hawayakubali wanalalamika kwamba iwapo watakubaliana na mafundisho yanayoshikilia amani na usalama basi watu wanaowazunguka watawaangamiza.

Uislamu unafundisha amani, na kama baadhi ya vikundi vya Kiislamu havitekelezi fundisho hili basi ni bahati yao mbaya. Kwa hakika hawayazingatii mafundisho ya Quran tukufu.

Hili ndilo jambo ambalo Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) na Jumuiya yake watalifanya. Ni lazima tuionyeshe dunia na hasa wale walio dhidi ya Islam kwa maneno yetu na matendo yetu kwamba Islam si dini hatari. Kama Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivyosema kwamba ni uongo na uzushi wa nguvu zilizo kinyume na Islam ambazo zinauweka ulimwengu kwenye hatari. Mataifa makubwa pia yanao mkono wao kwenye hali ya fujo na vurugu zinazoendelea katika mataifa ya Kiislam.

Baadhi yao sasa wanakiri kwamba makundi ya Waislamu wenye misimamo mikali ni zao lililopandwa na mataifa ya Magharibi huko Iraq. Wale wote wanaofanya ugaidi kwa jina la Islam, bila shaka wanafanya makosa makubwa lakini mataifa yenye nguvu nayo yamechangia sana katika kuukoleza moto huu. Haya yote yametokea kwa sababu haki na adili haifuatwi.

Zama zimebadilika na sasa si kila kauli itolewayo na mataifa makubwa kwamba inapokelewa na dunia yote. Kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kila mchunguzi wa mambo anaweza kuifikia dunia na kuwasilisha maoni yake. Kwa upande mmoja kuna mazungumzo ya kuuangamiza ugaidi kupitia mashambulizi ya anga lakini kwa upande mwingine wale wanaowapa nguvu magaidi hao au wanaofanya nao biashara ya fedha nyingi hawatiliwi maanani.

Amani ya dunia haiharibiwi na makundi ya Waislamu wenye misimamo mikali tu, ambao bila shaka wanasababisha hofu huku wakienda kinyume na mafundisho ya Islam; Lakini mataifa yenye nguvu kubwa nayo pia yanachangia sana katika uvunjfu huo wa amani. Kutimiza matakwa ya uchu wa ubinafsi kunaonekana ndilo jambo la mbele zaidi na amani ya dunia linafatia baadae.

Muislamu wa kweli anajua kwamba Mungu ni Salam (Chanzo cha Amani) na Anataka amani na usalama kwa viumbe vyake. Miongoni mwa Waislamu wakweli bila ya shaka Waahmadiya wanao ufahamu kamili wa amri na muongozo wa Mwenyezi Mungu kuhusu kutoa amani na usalama kwa binadamu na kustawisha amani duniani. Anasema hivi:

Na usemi wake (wa kila) mara ni: Ee Mola wangu, kwa yakini hawa ni watu wasioamini. Basi waache na useme: Amani. Hivi karibuni watajua. (43: 89-90)

Haya ni mafundisho ya Qur'ani tukufu. Wakati Mtukufu Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) aliwaita watu kwa Mungu, walikataa ujumbe wake. Si tu kwamba wao walikataa ujumbe wake wa amani, bali walijaribu kuharibu amani yake pia. Hata hivyo Mwenyezi Mungu akaamuru wasamehewe kwa sababu wao hawakuwa na uelewa na hawakuwa wenye busara na akamtaka Mtume (rehema na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) kuendelea kuwaambia kuwa ujumbe wake ulikuwa wa amani na usalama. Kwa kuangalia ni nini Mwenyezi Mungu alimuagiza Mtume (rehema na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) mbele ya uso wa mateso makubwa ya wapinzani, basi ni kiasi gani inakuwa muhimu zaidi leo kwa kila Muislamu kufuata nyayo hizo katika mazingira ya ulimwengu wa leo na kuubeba ujumbe wa Uislamu kwa wengine kwa njia hii.

Basi Kazi yetu ni kuusambaza ujumbe wa amani na usalama. Kama vile Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alivyosema: Hata kama isemwe nguvu ilitumika katika Uislamu basi ilikuwa ni katika kujilinda na kustawisha amani, na kamwe haikuwa kwa ajili ya kufanya ukatili. Ni jambo lililo mbali kabisa na ukweli kwamba Qur'ani imewahi, mahali popote kutoa amri ya kutumia Upanga / matumizi ya nguvu dhidi ya wale ambao hawakubali haya tunayo yasema. Kama vikundi vya Kiislamu au viongozi wa Kiislamu wanafanya matendo yaliyo kinyume na mafundisho ya Islam ya amani, basi hilo si kosa la Uislamu, ni kosa la maslahi yao binafsi au maslahi ya mataifa makubwa duniani ambayo wamewafanya watu hawa kama zana zao.

Pamoja na fundisho hili, Islam bado inadaiwa kuwa na mafundisho ya vurugu!

Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao husema: Amani;! (25:64)

Hili ndilo ambalo Qur'ani inalifundisha. Haitakiwi awepo hata mmoja wetu, hasa vijana, anayepaswa kuwa na aina yoyote ya utata. Ni Uislamu na Uislamu pekee tu ndio unaotoa dhamana ya amani katika dunia ya leo na Qur'ani pekee ndiyo inayotoa mafundisho ya kukomesha siasa kali/misimamo yenye kuchupa mipaka. Sisi sote tunahitajika kupata ufahamu wa mafundisho haya na kuyaweka katika matendo yetu ya kila siku na kama Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alivyosema: Ionyesheni dunia kwa matendo yetu kwamba leo Mwenyezi Mungu ametuwezesha kuilinda Qur'ani na hii ni fadhili ya Mungu tu. Ufafanuzi na maelezo Sahihi ya Qur'ani ni kulinda maana yake na Mungu amemtuma Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) kwa jambo hili. Mungu ametuwezesha kumkubali Masihi Aliyeahidiwa na hivyo ametuchaguwa sisi kuyaeneza mafundisho haya mazuri katika dunia. Ni wajibu wa kila Ahmadia. Kila Ahmadia mvulana, msichana, mwanamke na mwanaume anapaswa kufanya juhudi juu ya hili.

Dunia leo inaning'inia pembezoni mwa shimo la moto. Hali inaweza kutokea wakati wowote ambapo dunia inaweza kutumbukia katika shimo la moto. Ni wajibu wa kila Ahmadiya kujaribu kuiokoa dunia dhidi ya kuangukia katika shimo la moto na kufanya kazi kuelekea amani na usalama na ni Ahmadiya peke yake iwezayo kufanya kazi hii. Juhudi zinahitajika kwa ajili ya kazi hii. Kipengele kikuu cha kufikia lengo hili ni kuzalisha mahusiano maalum na Mungu, kugeukia kwake na kuinamia kwake na pia kupandikiza uchamungu na Utawa katika mioyo. Kisha ni hapo peke yake ndipo tutaweza kujipatia usalama na amani sisi wenyewe, kwa kizazi chetu kijacho na kwa dunia. Kwa ajili ya hali kama hii Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) aliwahi kusema katika ubeti mmoja wa shairi:

Ni moto, lakini wale wote wataokolewa kutokana na moto

Wale Wanaompenda Mungu, Mwenye Maajabu!

Kinachotakiwa hasa ni kukuza mahusiano yetu na Mungu Mwenye Nguvu, na kuyafanya mahusiano hayo kuwa yenye nguvu zaidi na kukuza upendo wetu Kwake. Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kujitahiudi kufanya hivyo na Awawezeshe watu wa kidunia kupata hisia za kumsikiliza Mungu ili nao waweze kujibadilisha na hatimae waweze kuokolewa dhidi ya kuanguka katika shimo la maangamizi.

Mwisho.

Kutimia kwa bishara ya Musleh Mauud

Kutoka uk. 2

sanamu nyingi. Alisema hii inaonyesha uponyaji wa magonjwa / matatizo kupitia baraka za Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu inaashiria roho ya Umoja wa Mungu. Pia alisema kuwa aliona katika ndoto kwamba yeye anakimbia na ardhi inanywea chini ya miguu yake. Bila shaka, katika maneno ya ufunuo wa bishara hii pia yamo: 'Atakuwa upesi upesi katika umbo' na Hadhrat Musleh Maud aliona katika ndoto kwamba yeye anazitembelea nchi nyingi duniani na ziara hizi bado hazikukamilisha kabisa kazi yake lakini yeye bado alikuwa na mipango ya kwenda mbali zaidi. Alisema aliona katika ndoto kwamba anasema: Ee mja mwenye shukrani kwa Mungu, mimi ninaendelea kwenda mbele na nitafanya tathmini baada ya kurudi safari yangu kama umoja wa Mungu umesimamishwa hapa na kama matendo ya kumshirikisha Mungu yamewachwa na kama mafundisho ya Uislamu na Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) yamemakinishwa katika mioyo! Bishara pia ilisema: "Atajulikana mpaka pembe za dunia', kwa hakika, maneno hayo yametimizwa kwa adhama kubwa.

Hadhrat Musleh Maud (r.a.) pia alifafanua vipengele vya bishara hii kupitia matukio mbali na ndoto hiyo.

Wakati aliposhika madaraka ya Ukhalifa watu walikuwa wakisema yeye bado ni mtoto. Anaeleza kwamba siku moja yeye alimsikia mtu akiwa pembezoni mwa msikiti akisema kwamba Jama'at ilikuwa inaharibiwa kwa mtoto kupewa nafasi kubwa. Alistaajabu kwamba ni mtoto gani wanayemkusudia. Baadaye alimuuliza mtu huyo katika msikiti ni mtoto gani aliyekuwa anamkusudia. Mtu yule alicheka na kusema kwamba mtoto ni wewe. Maneno haya ya mwenye kukashifu yalikuwa yanathibitisha maneno ya ufunuo, 'Atakuwa upesi upesi katika umbo' kwa sababu miezi michache baadaye watu hawa hawa waliokuwa wakimkosoa Hadhrat Musleh Maud walimsema kuwa anafanya hila. Ingawaje watu walimuona kuwa mtoto, lakini Mungu aliikabidhi ofisi hii ya kiroho kwake. Katika ofisi za kidunia, mtu anaweza kutumia nguvu, uwezo, utajiri na mengi zaidi lakini yeye alipewa ofisi ya kiroho katika wakati ambao senti chache tu ndizo ziliwachwa katika hazina ya Jamaat na deni kubwa lilikuwa limekusanyika.

Wale waliohusika na hali hii wote walikuwa wakimfanyia vurugu, ambao baadhi yao walikuwa wakisema kwamba kwa vile wao wameondoka, karibuni Wakristo watachukua milki ya jengo la Madrassa huko Qadian.

Katika suala la nyenzo za kidunia hakukubakishwa kitu chochote na wavurugaji walikuwa na furaha na kusema kwamba zama za yule ambaye amepewa ofisi zilikuwa zinapungua. Inaweza kufikiriwa ni hali gani iliyokuwa nayo Jumuiya katika nyakati hizo. Hata hivyo, hali ilivyokuwa siku za nyuma na wakati huo ambao Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alikuwa akiongea zilikuwa ni dunia tofauti na Jumuiya ilikuwa imeongezeka mara mamia zaidi na ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ulishafika nchi kadhaa za dunia na hazina ambayo iliwachwa ikiwa na senti chache ilikuwa sasa imejazwa na mamia ya maelfu! Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema hata kama mimi nifariki sasa hivi nitakuwa nimewacha nyuma yangu mamia ya maelfu ya watu na pia nitakuwa nimewacha nyuma yangu elimu kubwa. Hivyo bishara ya kiungu 'Atakuwa upesi upesi katika umbo' ilitimia kwa muonekano wa ajabu sana.

Wakati huo Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) alipotangaza bishara hii maadui zake walikuwa wakimshambulia kutoka kila upande. Hii ilikuwa ni kutokana na ukweli kwamba alikuwa amedai kuwa mpokeaji wa wahyi wa Allah. Yeye alikuwa bado hajatoa madai kuwa Mujjadid (Mhuishaji wa Dini) wala hakuwa ametoa madai ya kuwa Masihi. Ni wakati huo yeye alipoeleza bishara hii juu ya kupata mwana ambaye angekuwa na sifa za hali ya juu kabisa. Wakati sifa ya naibu wa mtu inavuma hiyo inaashiria sifa ya bwana (anayemwakilisha). 'Umaarufu' unaotajwa katika bishara hii unaashiria kwamba kupitia Musleh Maud jina la Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) litafika duniani kote.

Hadhrat Musleh Maud alisema, hayo yalitimia kwa utukufu mkubwa. Wakati wa uhai wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) ujumbe wake ulikuwa umefika Afghanistan tu kwa hali ya kutajwa. Katika maeneo mengine ni habari tu za ujumbe wake ndio zilikuwa zimefika. Khawaja Kamal ud Din alikuwa amekwenda London lakini yeye alikuwa na maoni kwamba, sio Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) wala Jama'at inayostahili kutajwa kwa majina yao huko, kwa hiyo ni jina lake tu ndilo lilikuwa linajulikana huko London. Hata hivyo, wakati Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alipokuwa Khalifatul Masih ujumbe ulipelekwa Java, Sumatara, China, Mauritius, nchi za Afrika, Misri, Palestina, Iran, nchi nyingine za Kiarabu na nchi za Ulaya. Katika sehemu nyingi wanajumuiya walikuwa ni kwa idadi ya maelfu na barani Afrika Wanajumuiya walikuwa kwa mamia ya maelfu.

Bishara pia ilisema: [yeye] atajazwa na maarifa ya kidunia na kiroho '. Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema hakuwa na tabia ya kufanya madai lakini hakuweza pia kuficha ukweli kwamba Mwenyezi Mungu alimsaidia kuandika na kuzungumza juu ya masuala yanayohusiana na Uislamu ambayo yalihitaji ufafanuzi sawa na wakati uliopo sasa na angeweza kudai kuwa kama maandiko hayo yawachwe pembeni, basi uenezi wa Uislamu duniani kote lingekuwa ni jambo lisiloweza kufanyika. Alisema kulikuwa na mambo mengi katika Qur'ani ambayo watu wasingeweza kuyaelewa kwa kuzingatia zama wanazoishi isipokuwa kama mambo hayo yangeelezwa kwa kuangalia mazingira ya aya zingine. Alisema ni neema ya Mungu kwamba tatizo hili lilikuwa lije kutatuliwa kwa njia yake. Alisema Islam ilikuwa inapita katika kipindi dhaifu na tete na kupitia Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) ulinzi wa Uislamu ulikuwa umeimarishwa tena. Hata hivyo, katika maisha ya Masihi Aliyeahidiwa kulikuwa hakuna mashambulizi ya kiutamaduni yaliyofanywa dhidi ya Uislamu kama ilivyokuwa katika wakati wake. Hivyo Mwenyezi Mungu Alipenda, kwa mujibu wa bishara ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s.), kumuinua mtu kwa mujibu wa Neno lake, mtu ambaye alikuwa na baraka ya Roho Mtakatifu pamoja naye. Mtu ambaye alikuwa amejazwa na elimu ya kiroho na kidunia na ambaye atayajibu mashambulizi ya kiutamaduni ya wapinzani kwa mwanga wa fafanuzi za Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) na adhama ya Qur'ani Tukufu na hivyo kulindwa Uislamu! Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu alivyoyapa kibali maandiko ya Hadhrat Musleh Maud (r.a.).

Hadhrat Musleh Maud alisema mpaka pale Mungu alipomjulisha kwamba kwa hakika yeye alikuwa ndio dhihirisho la bishara ya Musleh Maud, alikaa kimya na alizungumza tu wakati Mungu alipomwambia awaambie wengine. Alisema kwa neema yake Mungu, aliumba mazingira ambayo yanawiana na bishara hiyo. Watu wengi walipata ndoto ambazo somo la ndoto kumhusu Musleh Maud lilijirejea mara kwa mara. Mtu mmoja aliona kwamba malaika anaita jina la Hadhrat Musleh Maud na kutangaza kwamba jina lake litaandikwa pamoja na majina ya Manabii wa Mungu. Ndoto ya mtu mwingine ilimuona Hadhrat Musleh Maud akiwa amesimama juu ya mnara na kutangaza 'Je Allah Hamtoshei mtumishi Wake? ...' (39:37) Huu bila shaka ulikuwa ni mmoja wa funuo za mwanzo za Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) na kutangaza kutoka juu ya mnara kunaashiria kwamba Mwenyezi Mungu atauimarisha zaidi uenezi wa Ahmadiya kupitia Hadhrat Musleh Maud.

Akifafanua moja ya ndoto zake mwenyewe, Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema alikuwa ameisimulia ndoto hii kwa marafiki zake wachache wakati wa kuiona kwake, ambapo ilikuwa ni wakati wa miaka ya mwanzoni ya Ukhalifa wa kwanza wa Ahmadiyya. Aliona kwamba Sheikh Rehmat Ullah Sahib alishauri kutaka kujua nani ni mrefu, kati ya Maulawii Muhammad Ali Sahib na Hadhrat Musleh Maud. Ingawa Hadhrat Musleh Maud alikuwa anasita na hakutaka kuendelea, Sheikh Sahib alikuwa anamlazimisha. Katika hali halisi Maulawii Muhammad Ali Sahib alikuwa mrefu. Hata hivyo, wakati wao waliposimamishwa bega kwa bega katika ndoto Hadhrat Musleh Maud alionekana kuwa mrefu zaidi. Sheikh Sahib alitafuta meza na kumsimamisha Maulawii Sahib juu yake, lakini bado akawa halingani na urefu wa Hadhrat Musleh Maud. Sheikh Sahib kisha akaweka stuli juu ya meza na kumpandisha Maulawii Muhammad Ali juu yake. Hata hivyo, yeye bado akawa mfupi. Sheikh Sahib akamnyanyua Maulawii Muhammad Ali na kujaribu kumkweza ili afikie urefu wa Hadhrat Musleh Maud, lakini miguu yake ikawa inaelea hewani na urefu wake ukafikia mabegani mwa Musleh Maud. Hivyo Mwenyezi Mungu alimpatia taarifa ya mambo yajayo kwa njia ya ndoto yake hii. Ingawa wakati wa ndoto alikuwa ni Khawaja Kamal ud Din aliyekuwa akishindana naye kifua mbele na sio Maulawii Muhammad Ali, lakini katika ndoto Mungu alimuonesha kile kitakachokuja baadaye.

Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema hatimaye Maulawii Muhammad Ali Sahib alipungukiwa sana ikilinganishwa na Hadhrat Musleh Maud kiasi hiki kwamba nguvu yake yote ilitumika katika kushikilia kwamba mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu heshima iko kwa wale ambao ni wachache kwa idadi. Ingawa mwanzoni watu hawa walikuwa wakijisema kwamba wao wenyewe ni asilimia 95% na kuwasema wengine kwamba walikuwa ni asilimia 4% au 5% tu hivi, na kwamba hiyo ilikuwa inaashiria kuwa wengi wa Wanajumuiya wasingeweza kufuata upande wenye makosa. Wakati wa mfarakano ndani ya Jumuiya, Hadhrat Musleh Maud alipokea ufunuo 'Sisi tutawahafifisha na kuwafanya vipande vipande'. Watu hawa waliokuwa wakijiita wenyewe kuwa asilimia 95% kwa hakika walidhalilishwa na kuwa vipande vipande sawa na ufunuo wa Allah. Kabla ya kifo chake Khawaja Kamal ud Din aliandika, ufunuo ambao Mirza Mahmood aliwahi kuuchapisha kutuhusu sisi bila shaka umetokea kwa dhahiri nasi tumesambaratika na kuwa vipande vipande.

Hadhrat Musleh Maud (r.a.) alisema Mwenyezi Mungu mara nyingi Amejidhihirisha mwenyewe kwangu hivyo kutimiza [nyanja ya] bishara kwamba atakuwa na heshima ya Roho Mtakatifu wa Mungu.

Watu walimuuliza kuhusu hekima ya kuchelewa kutoa kwake tamko kwamba yeye alikuwa ndio dhihirisho la Musleh Maud ingawa marafiki wamekuwa wakiuhusisha utabiri huo kwake kwa muda mrefu kabisa.

Hekima iliyomo katika hili ni sawa na vile ilivyosemwa katika Qur'ani Tukufu:

'... Na Allah si Mwenye kuzipoteza imani zenu ...' (2:144). Wakati Mwenyezi Mungu anapowainua wale Anaoahidi kuwaleta baada ya ujio wa Manabii wake, Yeye huwa hataki kuliingiza kundi alilolianzisha katika ukafiri. Yeye anajenga mazingira ambayo wengi wa waaminio wanakuwa wako tayari kumkubali. Hadhrat Musleh Maud alisema wakati watu walipoziona bishara za Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) zinatimia katika dhati yake, imani yao iliimarishwa zaidi. Hekima ya kuchelewa kufanya madai hadi katika hatua ya baadaye ni kwamba Mungu hakutaka kuwaingiza waaminio wa kweli katika majaribio ya imani kwa mara ya pili. Hakutaka wao waingie kwenye uchungu wa huzuni mara mbili. Kwa hiyo, kwanza Mungu alimfanya yeye kuwa Khalifatul Masih na akaifanya Jama'at kuchukua kiapo cha utii (baiat) kwake na kisha akawezeshwa kutimiza ubashiri huu. Wakati ukweli ulipodhihirika mbele ya Jama'at kama ulivyo weupe wa mchana, na yule ambaye alikuwa ameahidiwa akapewa ufahamu wa kiroho kama vile ambavyo alipewa ufahamu wa elimu za kidunia ili mbingu na ardhi zote zimuunge mkono na waumini walindwe dhidi ya lawama ya kumkataa au kumkana.

Namuomba Mungu ailinde imani ya Waahmadiya. Sisi sote tufaidike na elimu ya kiroho ya Hadhrat Musleh Maud (r.a.) kama iwezekanavyo, ambayo bila shaka inapatikana katika lugha ya Kiurdu na lugha zingine pia. Ameen.

Bustani ya Washairi

MASHEHE MWASIKITISHA

Nyote muliopo sasa enyi mulowapinzani
Ambao mwamkanusha nabii wake manani
Huyo aliyetufika zama hizi duniani
Amabye kafananishwa kafanishwa na nani?
Kafananishwa na isa wa binti imraani

Ambaye ndiye hakika mrejeshaji undani
Kiroho ulotoweka halisi wa quran
Ili ipate huika upya dini ya manani
Ipate simama upya izishinde zote duniani
Umma wetu kwa hakika uondoke ujingani
Gizani upate toka urudi tena nuruni

Hivyo nawafahamisha mashehe wanazuoni
Huyo ,unomkanusha kiroho jieleweni
Nanyi mumerithi visa halisi vya makuhani
Tena wa zi mwaonesha nyinyi hasa fahamuni
Kuwa ndio ninyi hasa mulotamkwa zamani
Zama hizi kwa hakika mutapeleka motoni

Wazi wazi mwaonesha halisi hasa ni nyinyi
Ndio muliiotamkwa zama hizi duniani
Motoni mutapeleka kwa elimu za vichwani
Na ushahidi nawapa mulo nao eleweni
Ya kuwa ni ni ninyi hasa mupelekao motoni
Mabii mpya kafika huyo wa mola manani

Nabii huyo kafika nan a ushahidi rasmi
Mola alouonesha wa mbingu na ardhini
Ili kumthibitisha tuweze kumuamini
Kuwa ni nabii hasa si muongo abadani
Ni yule alotamkwa keshafika duniani
Bali munamkanusha mwapingana na manani

Nabii huyo kafika na ushahidi rasmi
Mola alouonesha wa mbinguni na ardhini
Ili kutusadikisha mola katia saini
Ni nabii hana shaka waja wangu mwaminini
Mwana Mariamu hasa ni huyo mpokeeni

Mwana mariamu hasa ni huyo mola manani
Mwenyewe kathibitisha leo wanazuoni
Wa makundi yakuzusha mwapingananan manani
Mwasema ushaisha utumewake manani
Mwishoni umeshafika huyo ni mtume gani
Munasema katakata huyo hamumuamini

Mwatisha mwasikitisha mashehe wanazuoni
Enyi muliopo sasa wa elimu ya vichwani
Mwasikitisha mwaogopesha mbaya wenu undani
Nabii mwamkanusha alotumwa duniani
Zam hizi kuhuisha upya dini ya manani
Kila hila mwapitisha watu wasimbaini

Munasema umeisha utume wake manani
Hivyo huyo alofika eti mtume wa nani?
Kumbe uongo mwazusha mkubwa uso kifani
Sababu ulioisha hasa ni utume gani?
Ni wenye sheria mpya huo ndio eleweni
Mwishoni uliofika hauletwi duniani

Lakini nawajulisha utume wake manani
Usio sharia mpya waendelea juweni
Na mola kathibitisha ho upo fahamuni
Maana huyo alofika zama hizi duniani
Alojitangaza hasa ni muhuishaji dini
Huyo munomkanusha mashehe wanazuoni

Huyo munomkanusha enyi wanazuoni
Alojitangaza tosha ni nabiiwa manani
Mola kamthibisha kwa ishara za mbinguni
Ili kutusadikisha ni kweli yake maoni
Abadani hajazusha katujulisha manani
Hivyo munomkanusha nazidi waelezeni

Enyi munomkanusha nabii huyo juweni
Kwa kusema umeisha utume wake manani
Muelewa vy kutosha elimu imewahuni
Hamunayo ninaapa ya isilamia dini
Ujinga unawatesa wa elimu ya vichwani
Uongo mwakithirisha unaotia motoni

Uongo mwakithirisha kwa elimu za vichwani
Hadithi mwazipotosha na kitabu cha manani
Undani mwabadilisha kwa fasiri za kubuni
Hivyo muelewe tosha mumezama uasini
Uasi mkubwa hasa unaosaliti dini
Musipojisahihisha kutubia kwa manani

Musipojisahihisha kutubia eleweni
Ahera mutaja juta nawambia zindukeni
Hasara itawafika kumalizia motoni
Maana hakimwapotosha mwaitia batilini
Kwa elimu za kuzusha nabii mwamfitini
Bado nasaha nawapa iwapo muujingani

Name nasaha nawapa nazidi wanasihini
Iwapo kweli hakika mashehe muujingani
Nawaapia naapa huyo musomuamini
Ni nabii hana shaka ametumwa na manani
Dini iliyotoweka ikahama umatini
Aturejeshee upya ili tutoke gizani

Hivyo nasaha nawapa mashehe wanazuoni
Enyi munomkanusha huyo muhuisha dini
Jiwahini kwa haraka tubieni tubieni
Ili apate ridhika mola awe radhi nanyi
Uradhi apate wapa awasamehe na nyinyi
Ili mupate okoka mujitowe hasarani

Ili mupate okoka mujitowe uasini
Uasi ule hakika wa ibilisi sheitani
Ambao mumerithishwa mashehe wanazuoni
Wa makundi ya kuzusha yalosemwa ya motoni
Yenye elimu za vichwa zinazopotosha dini
Tubieni kwa haraka mwombeni radhi manani

Bali nasaha nawapa mashahe tafakarini
Ili muviwache visa halisi vya makuhani
Walivyovitenda hasa kumtendea manani
Kwao vilosababisha wengi wangie motoni
Nanyi mumerithi hasa mujuwe huo undani
Tubieni kwa haraka mulobaki duniani

Viwacheni hivyo visa kiroho vya usheitani
Nanyi mulivyorithishwa halisi vya makuhani
Viongozi hasa hasa wale wakuu wa dini
Wa isiraili hasa walomuasi manani
Masihi wao kufika wakakosa muamini
Wakamtenda na visa vingi vya kumfitini

Wakatenda vingi visa kiroho kumfitini
Ambavyo mumerithishwa wasasa wanazuoni
Wanazuoni hasa ewa makundi ya motoni
Wenye elimu za vichwa zinazosaliti dini
Ambao mwanikanusha masihi8 wenu na nyinyi
Huyo aliyetufika zama hizi duniani

Ambao mwafahamishwa kuwa mumo uasini
Mahubiri munapata na tena ya kila fani
Madhumuni nanyi hasa muondoke ujingani
Nuru isharudi upya musibakie gizani
Haki sasa ishafika musibaki batilini
Bali la kusikitisha mumezidi upinzani

Hiyo ndo hatari tosha inayowakabilini
Lakusema mutakosa mbele ya mola manani
Maana munafahamishwa ili mujuwe undani
Muhuishaji kafika wa isilamia dini
Upya kaja kufundisha kitabu ch qurani
Ili kutuelimisha tuijuwe upya dini

Bali mukifahamishwa mashehe wanazuoni
Wa makundi ya kuzusha hayo yote ya motoni
Hamutaki mwakanusha munayopewa maoni
Mwamkana katakata huyo muhuisha dini
Ni kafiri munamwita hamutaki muamini
Viburi munazidisha kumtendea manani

Kila mukieleweshwa nabii mumbaini
Viburi munazidisha vya elimu ya vichwani
Kwa hivyo nawajulisha haina karaha dini
Mimi nawafamisha muzudi juwa undani
Muonyaji keshafika ametumwa na manani
Yule aliyetamkwa kuja akhera zamani

Muonyaji keshafika kutunusuru juweni
Elimu kairejesha halisi ya qurani
Dini ipate huika tuondoke ujingani
Gizani tupate toka umma urudi nuruni
Hivyo munomkanusha huyo musomuamini
Mukizidi mkanusha hiari yenu juweni

Mashehe nawajulisha huyo muhuisha dini
Kuhubiri nazidisha ni nabii wa manani
Mukizidi mkanusha hiari yenu na nyinyi
Nazidi wafamisha haina karaha dini
Litakiwalo hakika nanyi mujuwe undani
Yule nabii kafika alotamkwa zamani

Litakwalo kwa hakika nanyi mujuwe undani
Nabii yule halisa alotamkwa zamani
Alofanana na isa keshafika duniani
Hivyo mukimkanusha mashehe wanazuoni
Viburi mukizidisha vya elimu ya vichwani
Katu hamutookoka mbele ya mola manani

Bimkubwa Kombo, Zanzibar

MWANDANI

Bismillahi Manani, nianze kwa zako sifa
Miye wako insani, nijalie zako sifa
Na bongo langu kichwani, ulijaze maarifa
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Nazile zako sahifa, kuzichapa kitabuni
Nimfuate khalifa, nitambue kwa makini
Nitangaze taarifa, za Masihi Kadiani
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Ewe Mola wa Uchina, niongoze miye duni
Nifikishe na Madina, nikazuru arabuni
Niondolee ujana, nipatie na mwandani
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Mwenye sifa zilofana, uliyemvika dini
Akupendeze rabana, kila jiha zote fani
Kwa Masihi fungamana, amtangaze wodini
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Na jembe kulisakata, si mvivu asilani
Asimshike makata, kumuingia kichwani
Na rumba kulisakata, mbiombio masokoni
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Ya rabi ya rahamani, muepushe wale nyuni
Atulie jahazini, aweze fika ng'amboni
Asihofie majini, wasimamao njiani
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Ewe Mola nighofiri, miye wako masikini
Izara kuifikiri, niepushe wafitini
Nisiwe bora msafiri, njiani niwe makini
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Kaditama nimefika, nane beti zimetimu
Na sofani nainuka, naweka chini kalamu
Twakuimba msifika, pokea yetu kalamu
Ewe Mola wa ghofira, utuweke rehemani.

Al-Ustadh Ally Suleiman Magana – Pongwe, Tanga (The new big boss)

‘Hifdh Class’ yaanza kutoa matunda

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu mwanafunzi wa kwanza wa Darsa la Hifdhul Quran kutoka Jamia Ahmadiyya Morogoro amehitimu masomo yake kwa mafanikio makubwa.

Mwanafunzi huyo Zafrullah Abdulrahman Mohammed, ametumia kipindi cha mwaka mmoja na siku thelathini na moja kuweza kufanikiwa kuhifadhi Quran yote. Baada ya kumaliza kuhifadhi mara ya kwanza sawa na taratibu za kuhifadhi Quran alipitia tena mara mbili akiwa anasikilizwa na mwalimu wake.

Darsa ya kuhifadhi Quran ilianzishwa mwaka 2014 katika Chuo cha Jamia Ahmadiyya Morogoro kama juhudi za kuwaandaa vijana wetu kuwa mahiri katika fani zote za elimu ikiwemo fani hii muhimu ya kuhifadhi Qurani.

Mbashiri makhsus kwa ajili ya kusimamia darsa hilo Sheikh Hafidh Mahmood aliletwa kutoka Pakistan.

Hadi sasa Darasa hiyo imeshapokea wanafunzi zaidi ya 10 tangu kuanzishwa kwake na kwa sasa jumla ya wanafunzi 8 wanaendelea na darsa hiyo chuoni hapo.

Kumweka mtoto sehemu maalumu na kumfanya ashughulike na uhifadhi tu huku akisaidiwa na walimu mahiri ambao wenyewe wamehifadhi Qurani yote ndio njia muafaka ya kumfanya mtoto ahifadhi Qurani tukufu kwa kipindi kifupi.

Wanafunzi wanaopokelewa kwa ajili darasa hii ya kuhifadhi hutakiwa wawe na sifa zifuatazo:
Yafuatayo yanafaa kuzingatiwa na mzazi anayetaka kijana wake akubaliwe kujiunga na Darasa la Hifdh:
1. Awe anajua kusoma Quran Tukufu (matini yake). Pia awe na mapenzi na shauku ya kuhifadhi Qur’an tukufu.
2. Awe na umri kati ya miaka 11 hadi miaka 14.
3. Awe na afya nzuri, awe na tabia njema na awe na uwezo wa kuishi hosteli bila ya wazazi wake.
4. Wakati wa usaili aje na barua ya uthibitisho wa Mbashiri wake wa mkoa pamoja na Rais wa tawi lake.
5. Atapewa mtihani wa kuhifadhi sehemu ya Qur’an tukufu pamoja na usaili na baada ya hapo ndipo itathibitishwa kupata nafasi au kukosa

Kuhifadhi Quran kwa ghaibu ni moja ya muujiza mkubwa wa Quran tukufu na mamilioni ya Waislamu katika historia nzima ya Uislamu wamehifadhi Qurani kuanzia tangu zama za masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. hadi leo.

Mwenyezi Mungu alisaidie darasa hilo la kuhifadhi Qurani na awasaidie wazazi kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo za kuwapeleka vijana Jamia ili waweze kufaidika na utaratibu huu maalum.

Baada ya kumaliza darsa hilo la kuhifadhi, kijana Zafrullah alifanyiwa dhifa ya kumpongeza katika familia yake na hili hapa ni shairi ambalo lililosomwa kwenye dhifa hiyo.

1. Mola Ilahi, Jina Lako tuanzie
Bismillahi, nyoyo zetu zifungue
Tumefurahi, kutukumbuka na sie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

2. Mola Ilahi, darasa isaidie
Kwa uswalihi, daima iendelee
Yeye futuhi, wengine wafuatie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

3. Mola Ilahi, kusoma asizembee
Kwa asubuhi, na jioni apitie
Lugha fasihi, hukumu asikosee
Zafrullahi, Mola umbarikie.

4. Mola Ilahi, Pweke akusujudie
Azistahi, Aya azikumbukie,
Zilo shabihi, zote msahilishie
Zafrullahi, Mola umbarikie.



Zafrullah Abdulrahman Mohammed ambaye amemaliza kuhifadhi Quran Tukufu kupitia darsa la Hifdh Jamia Morogoro

5. Mola Ilahi, kifua mkunjulie
Mno awahi, kwa haraka akomae
Wako Masihi, aje amtumikie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

6. Mola Ilahi, Mfanye akulilie
Njia sahihi, Ya Rabbi muangazie
Akusabihi, pia akutegemee
Zafrullahi, Mola umbarikie.

7. Mola Ilahi, taqwa ashikilie
Kwenye fiqhi, huko ndiko azamie
Istilahi, zote mrahisishie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

8. Mola Ilahi, twaomba mhurumie
Yenye falahi, karibu msogezee
Na makruhi, mfanye ayachukie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

9. Mola Ilahi, Wewe akushukurie
Asikebehi, watu asipuuzie
Na majeruhi, wote awasaidie
Zafrullahi, Mola umbarikie.

10. Mola Ilahi, Mwenyewe utuambie
Humfedhehi, kitabu ahifadhie
Wake wajihi, peponi uje unga’e
Zafrullahi, Mola umbarikie.

Kambi ya Nasrat Dar yafana

Na Lajna Imaillah, Dar es Salaam

Mnamo mwezi Desemba 2015, lajna Immaillah pamoja na Nasrat wa mkoa wa Dar es Salaam, walifanya shughuli ya kambi katika maeneo ya Kitonga, jijini Dar es Salaam. Kambi ilianza siku ya Ijumaa tarehe 25 mpaka tarehe 27 Desemba 2015. Lengo kuu la kambi hii lilikuwa; kuwapatia watoto hao wa kike wenye umri kuanzia miaka saba mpaka ishirini, elimu ya malezi yanayozingatia maadili ya Kiislam.

Kambi ilifunguliwa na katibu wa fedha – Taifa wa Lajna Immaillah bi Zena Nyange. Aliwafahamisha washiriki kwamba elimu ya malezi watakayoipata ni muhimu sana kwao, kwa maendeleo ya kiroho hivyo aliwaasa kuwa wasikivu na kuwataka washiriki barabara kabisa. “Mtakapomaliza kambi hii muwe mmeiva vizuri ili malengo ya kambi hii yaweze kutimia” alisema Bi Zena. Mada kuu za kambi zilikuwa:
i. Mwenendo na tabia njema
ii. Kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu
Siku ya kwanza ya kambi (yaani Ijumaa tarehe 25/12/2015), mafunzo yalianza saa 3:20 asubuhi. Mwenyekiti alikuwa Bi Zena Nyange ambaye aliongoza kikao cha kwanza. Bi Zena alifungua kikao kwa usomaji wa Kurani Tukufu, ndipo mada zingine zilifuata. Katika kujadili mada ya kwanza wanakambi walifafanua kwa njia ya mjadala katika vikundi. Mada zilijadiliwa kiundani kupitia mafundisho ya Kurani Tukufu, hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w), pamoja na mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Mada zilieleweka vizuri zaidi kwa msaada wa viongozi wa kambi ambao walitoa ufafanuzi wa kina wa vipengele vyote vilivyojadiliwa. Kambi iliahirishwa ilipofika saa 12:15 jioni baada ya kumalizika mambo yote yaliyotakiwa kufanyika siku hiyo ya kwanza.

Siku ya pili – Jumamosi tarehe 26/12/2015, kikao cha pili kilianza saa 3:00 asubuhi. Mada ya pili (kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu) ndio ilijadilwa siku hii. Mwenyekiti alikuwa Bi Aisha Mpogo akishirikiana na wawezeshaji wake. Mada hii nayo ilijadiliwa kwa utaratibu uleule wa vikundi. Viongozi wa kambi walichangia mawazo yao ili kuongeza uelewa kwa wanakambi. Viongozi waliwasisitizia wanakambi kuhusu utawa, uchamungu, heshima- kwa wazazi na mengineyo.
Kambi ilifungwa majira ya saa 11:00 za jioni na Naibu Sadr Lajna Taifa bi Zanana Omary. Aliwausia wanakambi kuyaweka moyoni mwao mafunzo yote waliyoyapata na kuwasisitiza kusimamisha sala na kuwatii wazazi wao kama mhimili wa uchamungu. Mwishowe aliongoza maombi ya kimyakimya na kufunga rasmi kambi.

Viongozi walioshiriki kuandaa kambi hii ni Sadr Lajna Taifa Bi Mwamini Kazema ambaye alishirikiana na majlis yake, Sadr Lajna Mkoa Bi Naomi Paul ambaye pia alishirikiana na majlis yake. Wengine ni lajna wa Kitonga ambao walishirikiana na wapishi, pia Mwalimu Mbawala alishirikiana na Khuddam katika shughuli za ujenzi wa eneo la kambi.

Kambi hiyo ilifuatiwa na safari ya kiutalii ambapo wanakambi walipata fursa ya kutembelea Dar es Salaam Zoo kwa lengo la kujifunza na kujiburudisha. Wanakambi walifurahi sana kuwaona wanyama ambao walikuwa hawajahawahi kuwaona. Kilichowavutia zaidi katika ziara hiyo ni kuwaona simba, chui, fisi na mamba wakubwa. Pia walifurahishwa kupanda ngamia na farasi.

Majlis Lajna Taifa na Mkoa wa Dar es Salaam inatoa shukurani za dhati kwa wazazi wote waliofanikisha ziara hii. Kwa wale ambao hawakujaaliwa kushiriki kambi na ziara ya Dar es Salaam Zoo wanaombwa waanze maandalizi mapema ya kambi ijayo kwani haya yote ni kwa mafanikio ya watoto wetu na tanzim ya Lajna Immaillah - Amiin.

Muongozo juu ya Nidhamu ya kujitolea mali katika Jamaat Ahmadiyya

Allah anasema katika Qur'an tukufu:
... Na mali yoyote muitoayo, ni kwa (faida ya) nafsi zenu, wala msitoe ila kwa kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu; na mali yoyote mtakayotoa mtarudishiwa sawasawa, wala hamtapunjwa (2:273).

Hapa chini inaelezwa kwa muhtasari juu ya baadhi ya michango muhimu pamoja na kima chake sawa na mwongozo wa Quran Tukufu, Sunna za mtukufu Mtume s.a.w. maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. au makhalifa wake.

ZAKA
Zaka ni nguzo ya tatu ya dini ya Kiislamu na utoaji wake ni tendo la faradhi. Zaka ni neno la Kiarabu na maana yake ni kutakasa au kuzidisha. Na kile kinachotolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa shabaha ya kutekeleza nguzo hii, pia huitwa Zakat. Ni jambo la lazima kwa kila mwanajumuiya (Muislam) aliye 'SAHIB NISAB' kutoa zaka hata kama anatoa michango (chanda) mingine yoyote, kwani hapana chanda inayoweza kuwa badala ya zaka. Michango kama vile chanda Aam/hisa Amad hustahili juu ya mapato ya kikazi, mshahara au biashara n.k., wakati ambapo zaka hustahili juu ya pesa taslimu au akiba ikaayo benki kwa mwaka mzima au johari na vitu kama vile vinavyooneshwa hapa chini endapo thamani yao ni kiwango cha 'NISAB' au zaidi:-

SAHIB NISAB ni mtu mwenye kuwa nazo tola 52.5 (Gramu 612.36) za madini ya fedha au tola 5 (Gramu 87.48) za dhahabu kwa muda wa mwaka mzima. Kama moja wapo ya madini hayo haifikii kiwango cha nisab (kiasi ambacho zaka huwa inawajibika) basi zitajumlishwa pamoja zote aina mbili katika hesabu ya kutafuta kiwango kinachostahili cha zaka. Kuhusu pesa taslimu, NISAB yake hutegemea (bei) ya madini ya fedha. Kwa mfano, kama bei ya tola moja ya madini ya fedha ni Tsh. 10,000/-, hapo thamani ya tola 52.5 inakuwa ni shilingi 525,000/-. Sasa, kama akiba ya mtu katika benki iwe ni shilingi 525,000/- au zaidi kwa mwaka mzima au awe na pesa taslimu zaidi ya kiasi hicho, basi yeye ni *Sahib Nisab* na anawajibika kulipa zaka. Kiwango cha zaka katika mifano hii yote ni sehemu moja ya arubaini (1/40).
Pia mazao ya kilimo na mifugo nayo yanatolewa zaka yanapofikia kiwango cha Nisab. *Kwa maelezo zaidi soma kitabu cha Zaka.*

MCHANGO WA KAWAIDA WA KILA MWEZI (CHANDA AAM)
Mchango huu hutolewa kila mwezi na ni sehemu ya kumi na sita (1/16) ya kipato cha kila mwezi. Kwa mfano:-
Kama kipato cha kila mwezi ni Tsh. 100,000/- (laki moja), basi Chanda Aam itakuwa Tsh. 100,000 ÷ 16 = 6,250 kwa mwezi.

MCHANGO WA CHANDA JALSA SALANA (MKUTANO WA MWAKA)
Mchango huu hutolewa mara moja kwa mwaka kwa kiasi cha sehemu ya 1/120 ya kipato cha mwaka mzima. Kwa mfano:- Kama kipato cha mwaka mmoja ni Tsh. 1,200,000/- (yaani Tsh. 100,000/- kwa mwezi), Chanda Jalsa Salana itakuwa Tsh. 10,000/- kwa mwaka. Kwa kurahisisha mahesabu ya mchango huu mtu anaweza kulipa 1% ya mapato yake ya kila mwezi.

MCHANGO WA CHANDA WASIYYAT-
WATU WALIOFANYA WASIA
Mchango huu unazo sehemu mbili: HISSA AMAD na HISSA JAIDAD. Hissa Amad, hutolewa kila mwezi na Mwanajumuiya aliyemo kwenye mpango wa Wasia. Kiwango chake ni baina ya sehemu moja ya kumi (1/10) na theluthi moja (1/3) ya kipato cha muusi, sawa na kiwango alichoahidi katika wasia wake. Hissa Jaidad, hutolewa na Muusi sawa na kanuni za wasia, nayo ni sehemu moja ya kumi (1/10) hadi theluthi moja (1/3) ya mali (rasilimali) ya Muusi sawa na kiwango alichoahidi katika wasia wake. Kwa maelezo zaidi, someni kitabu cha Wasia.

MCHANGO WA - CHANDA TAHRIK JADID
Mchango wa Tahrik Jadid au 'mpango mpya' ulianzishwa hapo mwaka wa 1934 na Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Khalifatul Masih wa pili r.a. ili kugharimia uenezaji wa Islam katika nchi zilizo nje ya India. Mchango wa Tahrik Jadid hutolewa mara moja kwa mwaka sawa na ahadi ya mtu. Mwaka wa Tahrik Jadid huanzia tarehe mosi mwezi wa Novemba hadi mwaka unaofata tarehe 31 mwezi Oktoba. Mwaka wenyewe kwa kawaida hutangazwa na Hadhrat Khalifatul Masih akiwanasihi wanajumuiya wote kutoa ahadi zao za kuuchangia mpango wa Tahrik Jadid kwa ukarimu. Bali watoto pia washirikishwe katika mchango huu. Wakati wa kuleta ripoti ya ahadi za Tahrik Jadid ni muhimu pia kutaja namba ya daftar ya kila mtoa ahadi.

Ufafanuzi kuhusu Daftar
Namba ya Daftar humaanisha ni mwaka gani mtu alianza kulipa mchango wa Tahrik Jadid sawa na vipindi vya miaka iliyopangwa kama ifuatavyo:

Daftar 1	1934 - 1944
Daftar 2	1944 - 1965
Daftar 3	1965 - 1985
Daftar 4	1985 - 2004
Daftar 5	2004 - Sasa

MCHANGO WA - CHANDA WAQFE JADID
Kama ulivyo mchango wa Tahrik Jadid, mchango wa Waqfe Jadid nao pia ulianzishwa na Hadhrat Khalifatul Masih wa Pili r.a. hapo mwaka wa 1957. Mchango huu hutolewa mara moja kwa mwaka na kiwango chake ni sawa na ahadi ya mtu aliyoweka. Shabaha ya mchango huu ni kugharimia mpango wa kuelimisha Wanajumuiya wa vijijini na kuwahubiri wasio Waislamu.
Hapo awali mpango wenyewe ulikuwa uwaelimishe kidini wanajumuiya wa Pakistani na kuwahubiria Mabaniani wa nchi hiyo na ilikuwa ni wanajumuiya wa kule peke yao waliowajibishwa kutoa mchango huu wa Waqfe Jadid. Lakini baada ya mpango huu kupata ufaulu mkubwa kwa fadhili za Allah, Hadhrat Khalifatul Masih IV r.a. aliupanua mchango huu na kuwashirikisha wanajumuiya kote ulimwenguni, na watoto pia.
Mwaka wa Waqfe Jadid hutangazwa na Hadhrat Khalifatul Masih na huanzia tarehe mosi Januari hadi tarehe 31 mwezi wa Disemba. Kama vile ilivyo kuhusu mchango wa Tahrik Jadid, majina ya wanaoahidi kuuchangia huwa yanapelekwa kwa Hadhrat Khalifatul Masih ili kuwaombea. Sawa na mwongozo wa Markaz idadi ya wachangiaji wa mchango huu wenye umri ulio chini ya miaka 12 hutakiwa itofautishwe na ile ya walio na umri unaozidi miaka 12.

FIDIA YA SAUMU
Iwapo mtu ameshindwa kufunga saumu kwa sababu za kisheria (kama vile ugonjwa na safari) anatakiwa kulipa fidia kwa siku alizoshindwa kufunga. Kiasi cha fidia ni chakula cha kuweza kumlisha maskini mara mbili kwa siku. Amiri au Mbashiri mkuu wa nchi, huweka kiwango cha fidia sawa na hali ya nchi ilivyo.
Ni vyema ieleweke kwamba hata kama mtu ametoa fidia lakini baadae dharura iliyomzuia kufunga saumu ikaondoka anatakiwa azifunge siku zile ambazo aliacha kufunga.

FITRANA (ZAKATUL FITRI)
Mtume s.a.w, amewalazimisha Waislamu wote wanaume kwa wanawake, na hata watoto wachanga, kutoa Fitrana wakati wa sikukuu ya Id-ul-fitri. Kwa kawaida kiwango cha Zakatul fitri ni ratili nane za nafaka kwa kila mtu mmoja. Hata hivyo ni kawaida katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa Amiri au Mbashiri mkuu wa nchi, kuweka kiwango cha Fitrana sawa na hali ya nchi ilivyo. Fitrana hukusanywa chini ya usimamizi wa Amiri wa Jumuiya ambaye huhakikisha kuwa inagawiwa kwa wale wanaostahili ili nao waweze kusherehekea Idi kama ndugu zao wengine. Na hii fitrana itolewe kabla ya kusali sala ya Idul Fitri ili wale wasiobahatika wapewe ili washerehekee sikukuu pamoja na wale wengine.

MFUKO WA SIKUKUU YA IDI (EID FUND)
Mfuko wa sikukuu ya Idi huchangiwa wakati wa Idi zote mbili - Idi Kubwa na Idi Ndogo. Yapendekezwa sana kwa mtu kuchangia kabla ya kusali sala ya Idi. Kiwango chake hukadiriwa na Amir wa Jumuiya sawa na hali ya nchi ilivyo. Matumizi ya fedha za mfuko huu husimamiwa na Hadhrat Khalifatul Masih.

SADAKA
Kutoa sadaka ya hali na mali ni Sunna ya Mtume s.a.w. Yeye alikuwa ni mkarimu kupita wanadamu wote na katika Mwezi Mtukukufu wa Ramadhani yeye alizidisha sana ukarimu wake kwa kutoa sadaka kuwasaidia masikini na wasiojiweza na wale wenye shida mbalimbali. Katika hadithi moja Hadhrat Ibn Abbas r.a anasimulia ya kwamba; Mtume s.a.w ndiye aliyekuwa mkarimu kupita watu wote na ukarimu wake ulizidi sana katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ambapo Hadhrat Jibril a.s alimjia kila siku usiku na kumsomea Qur'an tukufu. Katika wakati huu wa Mwezi wa Ramadhani ukarimu wa Mtume s.a.w ulizidisha mwendo kupita upepo uletao mvua. (Bukhari na Muslim). Sadaka haina kiwango maalumu na kila kitu nafaka, mavuno mengine ya shambani, mifugo, pesa, n.k chaweza kutolewa sadaka. Katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya sadaka hukusanywa chini ya usimamizi wa Amir wa nchi na matumizi yake husimamiwa na Hadhrat Khalifatul Masih.

MICHANGO YA MAJLIS ANSARULLAH
1. Chanda Majlis: Mchango huu hulipwa na kila Ansar (Mwanajumuiya mwanamume mwenye umri wa miaka 40 na zaidi) pamoja na michango mingine tuliyoitaja. Kiwango chake ni Asilimia moja (1%) ya kipato cha kila mwezi.
Kwa mfano: Kipato cha mwezi mmoja = Tshs. 500,000/-
Chanda Majlis itakuwa = Tshs.5,000/-

2. Chanda Ijtima. Mchango huu halikadhalika hutolewa na kila Ansar pamoja na michango mingine iliyo tajwa. Kiwango chake ni asilimia moja na nusu ya kipato cha mwezi mmoja kwa mwaka.
Kwa mfano: Kipato cha mwezi mmoja = Tsh. 500,000/-
Chanda Ijtima itakuwa = Tsh. 7,500/- kwa mwaka.

MICHANGO YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA
1. Chanda Majlis Khuddamul Ahmadiyya. Mchango huu hutolewa na kila Khadim (kijana wa miaka 15 mpaka 40) pamoja na michango mingine iliyotajwa. Kiwango chake ni asilimia moja (1%) ya kipato cha kila mwezi.
Kwa mfano: Kipato cha mwezi mmoja = Tshs. 450,000/-
Chanda Majlis Khuddam itakuwa = Tshs. 4,500/-

2. Chanda Ijtima. Mchango huu halikadhalika hutolewa na kila Khadim pamoja na michango mingine iliyo tajwa. Kiwango chake ni asilimia mbili na nusu ya kipato cha mwezi mmoja kwa mwaka.
Kwa mfano: Kipato cha mwezi mmoja = Tsh. 450,000/-
Chanda Ijtima itakuwa = Tsh. 11,250/- kwa mwaka.

MICHANGO YA LAJNA IMAILLAH
1. Chanda Lajna Imaillah. Mchango huu hutolewa na kila Lajna (kinamama kuanzia miaka 15 na kuendelea) pamoja na michango mingine iliyotajwa. Kiwango chake ni asilimia moja (1%) ya kipato cha kila mwezi.
Kwa mfano: Kipato cha mwezi mmoja = Tshs. 400,000/-
Chanda Lajna itakuwa = Tshs. 4,000/-

Tafadhali Zingatia:
Kwa ajili ya Chanda za Atfal na Nasirat; wanachama wa Majaalis zote wasio na kipato kabisa; wanafunzi; kinamama wa majumbani pamoja na Chanda Ijitimaa kwa ajili ya Lajna Imaillah, Majaalis husika kupitia vikao vyao vya Shura za Kitaifa, zitapendekeza kwa Hadhrat Khalifatul Masih juu ya kiwango wanachoshauri kichangiwe kwa kila kundi husika.

MICHANGO MINGINE
Mbali na michango iliyotajwa hapo juu, ipo pia michango mingine kadhaa ambayo wanajumuiya wanatakiwa kuchangia sawa na jazba zao za kiimani na sawa na uwezo wao kifedha. Michango hiyo ni pamoja na:
Mchango wowote unaoitishwa na Hadhrat Khalifatul Masih kwa ajili ya miradi maalum.
Mingine ni pamoja na: Mchango wa Maendeleo, Ujenzi wa Misikiti; Tahir Fund, Mariam Fund, MTA Fund, Mfuko wa Elimu; Sayyidna Bilal Fund, Local Fund, mchango wa Mengineyo; n.k.

WAJIBU WA KATIBU WA FEDHA

Kila aliye Katibu wa Fedha au katibu anayehusika na mchango fulani makhsusi, mfano: Tahrik Jadid, Waqfe Jadid n.k. anakumbushwa kuzingatia majukumu yake kuwa ni:-
1. Kukusanya ahadi au bajeti kutoka kwa wanajamaat katika wakati muafaka na kuzituma kwenye ngazi inayohusika.
2. Kwa upendo na mawaidha mema kuwakumbusha na kuwahimiza ndugu kutoa michango yao.
3. Kumpatia risiti ndugu yeyote mara tu anapotoa mchango wake.
4. Kuziwasilisha fedha alizokusanya katika Jumuiya sawa na miongozo aliyopatiwa na ngazi za juu.
5. Kuandaa ripoti za mwisho wa mwezi au mwisho wa mwaka na kuzituma katika ngazi inayohusika.
6. Kuweka rekodi ya kumbukumbu za taarifa zote za makusanyo ya michango katika matawi.

SHURA YA KITAIFA 2016

Amir Sahib - Jamaat Ahmadiyya Tanzania, anapenda kuwakumbusha Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, Marais wa matawi, Walimu wa Jamaat nchini na Wanajumuiya wote kwa ujumla kwamba sawa na Kalenda ya matukio ya Jumuiya ya mwaka 2014/15, Majlis Shura ya Kitaifa itafanyika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga - Dar es Salaam, siku za Jumamosi tarehe 30 April na Jumapili tarehe 01 Mei 2016.

Matawi yote yanatakiwa yafanye vikao vya kupendekeza ajenda za Shura pamoja na kuchagua wajumbe wa kuyawakilisha matawi yao kwenye Shura hiyo ya Kitaifa. Tawi lililo na wachangiaji zaidi ya 50, linaruhusiwa kuchagua mjumbe wa ziada kwa kila wachangiaji 50 wanaoongezeka.

Marais wote wa mikoa wanatakiwa washiriki.

Pamoja na mjumbe wa Shura atakayechaguliwa kutoka kila tawi, rais wa tawi naye pia anatakiwa ashiriki kwenye Shura ya mwaka huu.

Wajumbe wote wanatakiwa wawe wamefika kwenye eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam jioni ya siku ya Ijumaa tarehe 29 April 2016.

Pia tuzingatie kwamba, mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi hivyo ni muhimu kila tawi la Jumuiya lisipoteze nafasi yake ya kuleta mjumbe pamoja na ajenda kama watakuwa nayo.

MPANGILIO WA MASHINDANO YA IJTIMAA YA KHUDDAM 2016.

AINA YA SHINDANO		KHUDDAM	ATFAL
1. QURAN	(A) HIFDH	(i) JUZUU YA 30	(i) SURA MBALIMBALI (ii) JUZUU 30 (iii) JUZUU 29&30 (iv) JUZUU YA 27,28,29&30
		(ii) SURAT AS-SAF, 61:1-10 Na SURAT AL-JUMAA, 62:1-12	
	(B) TAFSIRI	(i) SURAT AN-NISAA, 4:61-71	(i) SURAT BAQARA, 2:17-21 (ii) SURAT AN-NUUR 24:56-58
	(C) TILAWAT	MSOMAJI ATAPEWA SEHEMU YOYOTE KUTOKA QUR'AN NA KUSOMA KWA KUFUATA KANUNI.	MSOMAJI ATAPEWA SEHEMU YOYOTE KUTOKA KATIKA QUR'AN NA KUSOMA KWA KUFUATA KANUNI.
2) HADITHI		KUHIFADHI NA KUTAFSIRI HADITHI ZA MTUME (s.a.w) KUTOKA KITABU CHA KIUNGA CHA WATU WEMA. HADITHI ZIFUATAZO. NAMBA 926 UK- 801, HADITHI NAMBA 938 UK-819 NA NAMBA 950 UK-835	(A) {i} HADITH AROBAIN PAMOJA NA MAELEZO YAKE, HADITH NO 1- 40**. (ATFAL WA MIAKA 11-14)** {ii} KUHIFADHI NA KUTAFSIRI HADITHI ZA KIUNGA CHA WATU WEMA, HADITH NO. 930, 931 NA 933. **(ATFAL WA MIAKA 11-14)**
			(B) HADITH AROBAINI BILA YA MAELEZO KWA MPANGILIO **(ATFAL WA MIAKA 7-10)**
3) HOTUBA		KICHWA CHA HOTUBA NI ***Islam na amani ya kweli ya ulimwengu*.** HOTUBA IONYESHE REJEA KUTOKA KATIKA KURANI TUKUFU, HADITH, KAULI ZA MASIH ALIYEAHIDIWA (A.S) PAMOJA NA MAKHALIFA WAKE.	ATFAL ACHAGUE KICHWA KIMOJA TU KATI YA VILIVYOPO NA AANDAE HOTUBA YAKE YA. **(i) *Umuhimu wa kuutii ukhalifa*.** **(ii) *Umuhimu wa kusimamisha sala*.**
4) SHAIRI		(i) **KUTUNGA SHAIRI PAMOJA NA KUGHANI**. SHAIRI LIWE NA KIBWAGIZO KIFUATACHO. "***Islamu ndiyo Nguzo, ya Amani duniani*"**	KUGHANI SHAIRI LA: ***Masihi Muahidiwa, amedhihiri na Shani*.**
		(ii) KUGHANI SHAIRI LA ***MSAADA WENYE SHANI***. KUTOKA KITABU CHA MWANA MKUU WA IBRAHIM UK-186.	
5) SALA YA KIISLAM		**SHINDANO LA SALA YA KIISLAM**. -MASWALI YATAULIZWA KUTOKA ***SEHEMU YOYOTE YA KITABU CHA SALA.***	(A) MASWALI YA VITENDO VYA SALA. **(ATFAL WA MIAKA 7- 10)**
			(B) MASWALI KUTOKA KATIKA SALA ZIFUATAZO: ALFAJIR, IJUMAA, WITRI, JENEZA, TARAWEHE, TAHAJUD NA IDD. **(ATFAL WA MIAKA 11-14)**
6) MAOMBI.		KUHIFADHI MAOMBI KUMI (10) *ALIYOYAAGIZA* HUZUR (ATBA). PAMOJA NA MASWALI KUTOKA KWENYE KITABU CHA MAOMBI YA QUR'AN KUANZIA ***NAMBA 1 HADI NAMBA 10 (1-10).***	KUTOKA KWENYE KITABU CHA MAOMBI YA MTUME (S.A.W). (i) DUA 31-40 - **(ATFAL WA MIAKA 7-10).** (ii) DUA 51-60 - **(ATFAL WA MIAKA 11-14)**
7) QUIZ.		MASWALI KUTOKA KWENYE MASOMO YA DINI, ELIMU YA SECULAR, HISTORIA YA JAMAAT NCHINI TANZANIA NA HISTORIA YA TANZIM YA KHUDDAM	MASWALI KUTOKA KWENYE MASOMO YA DINI, ELIMU YA SECULAR, HISTORIA YA JAMAAT NCHINI TANZANIA NA HISTORIA YA TANZIM YA KHUDDAM.

MICHEZO:

S/NO	KHUDDAM	ATFAL
1.	KUVUTA KAMBA	KUVUTA KAMBA
2.	KURUSHA TUFE	KUKALIA MAPUTO
3.	MPIRA WA MIGUU	MPIRA WA MIGUU
4.	RIADHA MBIO ZA RAUNDI 6	RIADHA - MBIO RAUNDI 3
5.	MIELEKA YA MEZANI	KUKIMBIA NA MAYAI KWA KUTUMIA VIJIKO MDOMONI
6.	LONG JUMP	REBOUNCE BALL (KUDUNDI*SHA* VIPIRA UKUTANI)
7.	VOLLEYBALL.	

ATFAL WOTE WANAOMBWA WAFANYE MAANDALIZI KATIKA SHAIRI LA "*MASIHI MUAHIDIWA, AMEDHIHIRI NA SHANI*".
SHAIRI HILO TAYARI LIMESHATUMWA MATAWINI KOTE.

Sheikh Inayatullah Khalil na mahaba ya Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru
– Dar es salaam

Ukurasa wa Masheikh wa mwanzo mwanzo kuja Afrika Mashariki, wakisifika na kuheshimiwa kwa vilemba vyao vyenye haiba kubwa unaelekea kufungwa na kifo cha hivi karibuni cha Sheikh Inayatullah Ahmad kilichotokea siku ya kumbukumbu ya uhuru wa nchi yetu tarehe 09/12/2015 ni kama kimeweka kituo kwenye sentensi ndefu iliyoanza mwaka 1934 chini ya utaratibu wa Tahrik-e-Jadid mpango wa kimbingu uliotangazwa na mwana aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra). Sifa moja inayowaunganisha Masheikh hao wa mwanzo ni mapenzi yao ya dhati kwa wenyeji wa Afrika Mashariki. Mapenzi yaliyowafikisha katika kutoa machozi. Mwaka 1988 Sheikh Mubarak Ahmad Mbashiri wa kwanza kutumwa Afrika Mashariki alipokuja kutayarisha safari ya Khalifatul Masihi –IV (rh) nchini Tanzania mara kwa mara alipokumbatiana na watoto wake wa kiroho alimiminikwa na machozi na kila mara alitoa zawadi na inasemekana ya kwamba alirudi London akiwa na pea moja tu ya suruali na shati. Na linalokumbukwa sana na wale waliokutana naye, neno la kwanza lililotoka kutoka kwake ni 'mwanangu'.

Sheikh Muhammad Munawwar aliwaambia watu waliokwenda kumtazama Rabwah–Pakistan ya kwamba siku zote njozi zake anazipata katika lugha ya Kiswahili. Na siku moja kuna mtu alikwenda kumjulia hali, mara alipogonga mlango wa Sheikh alijibiwa "Karibu tupo huku nyuma", hapo yule mtu alishikwa na mshangao Sheikh anaongea lugha gani tena!! Kwani mtu yule aliyekwenda kumjulia hali alikuwa sio Mswahili wala alikuwa hajawahi kufika huku Afrika ya Mashariki na kusikia Lugha ya Kiswahili ikizungumzwa.
Tukio jingine linaloonesha mapenzi ya Sheikh Muhammad Munawwar kwa wananchi wa Afrika Mashariki kwa ujumla ni pale alipotoa hotubayake ya mwisho katika Masjid Salaam kabla ya kwenda kuwa Mbashiri Mkuu nchini Nigeria. Katika hotuba hiyo ya mwisho alisema ya kwamba; Tafadhali nikifa niko hapa, tafadhali nipelekeni Temeke ili mnizike karibu na ndugu yangu akimaanisha Sheikh Kaluta Amri Abedi. Ni kweli walifanya kazi pamoja kwa takribani miaka 13 wakati wanatafsiri Kurani Tukufu. Na ni dhahiri pindi unaposoma maandiko ya Sheikh Munawwar yanafanana sana na Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Sheikh Inayatullah Ahmad Khalil aliipenda sana Tanzania na siku zote alikuwa anaomba apate fursa na apate afya ili aweze kuja kuwatembelea wanawe wa kiroho wa nchi hii. Na wazee wengi waliokutana naye wanatoa ushahidi ya kwamba hakuchagua chakula, chakula alichokuta wenyeji wanatumia alitumia hicho hicho kwa furaha bila manung'uniko ya aina yoyote. Na siku zote aliendelea yeye kujihesabu kwamba ni mwana wa nchi hii. Na matendo yaliyofuatia baadae na kutolewa ushahidi na wajumbe waliokwenda katika mkutano wa mwaka mjini London, akiwemo Mwalimu Alli Saidi Mosse, Mwalimu Omar Ali Mnungu, Alhaji Mohammed Kungulilo, Bw. Elias Marwa wote wanatoa ushahidi kiasi cha mapenzi ya Sheikh Inayatullah Ahmad kwa watu kutoka Afrika Mashariki. Miaka mingi alikuwa hatoki kitandani, na wote waliokwenda kumtembelea isipokuwa Khalifa Mtukufu hakuweza kusimama na kuwasindikiza. Lakini ujumbe kutoka Tanzania ulipoingia nyumbani kwake Sheikh Inayatullah Ahmad alionesha furaha ya aina yake na akainuka kutoka kitandani na kuketi. Alisimulia mambo mengi sana kuhusu miaka yake ya utumishi nchini Tanzania. Na kila alipowatazama wajumbe hao machozi yalitiririka kutoka usoni. Lakini lililoshtua kuliko yote jambo ambalo lilimshtua pia na mwanae Habibullah ni wakati alipodiriki kutoka nje na kuwafungulia mlango wajumbe kutoka Tanzania na kuwapungia mkono wa kwaheri!! Jambo hilo lilimfanya hata mwanae Habibullah kutokwa na machozi. Wakati akiwapungia mkono aliwaambia wafikishe salaam zake kwa Chifu Abdallah Saidi Fundikila pamoja na Chifu Adam Sapi Mkwawa. Alisema ya kwamba viongozi hao na viongozi wengi katika Tanzania waliheshimu sana Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya na waliheshimu sana mchango wa Jumuiyya ya Ahmadiyya katika maendeleo ya nchi.

Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

Kutoka uk. 12

takatifu, na ameepukana na uchafu wote. Ni nuru ya Allah. Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Atafuatana na rehema ambayo itawasili pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya Baraka za Roho ya kweli. Yeye ni Neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne (hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu, Jumatatu iliyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu; kama kwamba Allah Ameshuka kutoka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na atakuwa sababu ya kudhihirika kwa Jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa, nuru iliyosingwa na Mwenyezi Mungu uturi wa mapenzi Yake.Tutampulizia roho yetu atahifadhiwa chini ya Kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale waliomo utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishiwa na jambo hili limekwisha katwa" (Tangazo la tarehe 20 Februari, 1986).
Pia sehemu nyingine kuhusu bishara hii ilisema:

"Rehema itafika pamoja na kuja kwake. Yeye ni nuru na ni mabruk na mtakatifu na yu miongoni mwa watawa. Ataeneza Baraka na atawalisha watu chakula safi na atakuwa mwenye kuinusuru dini …. Atakuwa na ufahamu na akili na atakuwa mwenye kupendeza. Moyo wake utajazwa elimu, batini yake itakuwa na upole na kifua chake kitajazwa utulivu. Atajaaliwa roho ya Umasihi na atabarikiwa na roho mwaminifu. Jumatatu. Jumatatu iliyobarikiwa, roho za watu wenye Baraka zitafikwa kwako" (Aynai Kamalat Islam uk. 577 – 578).
Mada ya pili ilikuwa ni Kutimia kwa bishara za Mwana Aliyeahidiwa ambayo ilitolewa na Mwl. Abdallah Mbanga.
Mwl. Mbanga alitumia muda wake vizuri kwa kuwaeleza wasikilizaji jinsi ambavyo vipengele kadhaa vya bishara hiyo vilivyotimia kupitia Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmuud Ahmad r.a.

Mada ya tatu ambayo ilitolewa na Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Khurram Shahzad sahib ilikuwa ni Wajibu wa Ahmadiyya sambamba na bishara ya Mwana Aliyeahidiwa, ambapo sheikh sahib aliwaeleza wasikilizaji juu ya majukumu yetu kadhaa tunayolazimika kuyatimiza ili kuweza kufaidika na ujio huu wa Mwana Aliyeahidiwa.

Baada ya mada hizo, wasikilizaji pia walipata nafasi ya kuuliza maswali kuhusu bishara hii na majibu muafaka yakatolewa sambamba na maswali yaliyoulizwa.
Maadhimisho hayo yalihitimishwa kwa hotuba ya ufungaji iliyotolewa na Amir na Mbashiri mkuu maulana Tahir Mahmood Chaudhry, ambapo alielezea vipengele kadhaa vya bishara ya Mwana Aliyeahidiwa jinsi vilivyotimia katika dhati ya Hahdrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad. Alisema pamoja na kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ndiye mwasisi wa jamaat Ahmadiyya kwa Amri ya Allah lakini mfumo wote wa nidhamu ya uendeshaji wa Jamaat tulio nao sasa, kwa mfano mfumo wa uongozi, mfumo wa shura n.k. hivyo vyote vilianzishwa na Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, ambaye ndiye mwana Aliyeahidiwa. Amir Sahib alimalizia hotuba yake kwa kuwakumbusha wajumbe kwamba kuadhimisha kwetu siku kama hii ya Mwana Aliyeahidiwa kutakuwa na maana tu pale ambapo tutajitahidi kuishi maisha yetu sawa na mafundiaho ya Jamaat ambayo ndio Uislamu sahihi. Maadhimisho hayo yalihitishwa kwa maombi ya kimywa yaliyoongozwa na Amir sahib.

Sheikh Inayatullah na wanawe

Kutoka uk. 12

kichwani
Kajitoma kwa uzembe, si elimu asilani.

Sheikh Inayatullah Ahmad na Habibullah walifurahi sana kuwaona wageni toka Tanzania. Kwa muda kipande kile cha Uingereza kikawa Tanzania. Na haraka aliwatolea picha za maisha yake katika nchi ya Tanzania. Huku akiwaonesha picha aliwaambia; "Ninapenda sana Tanzania, ujana wangu wote nimeutumia Tanzania, ningelikuwa na afya ningemuomba Khalifa Mtukufu niendelee kufanya kazi Tanzania. Mapenzi yangu kwa Tanzania ni makubwa mno". Aliendelea kusema; "Kuna wakati nilipata njozi ya jambo la hatari lililokuwa karibu kutokea. Tulichinja ng'ombe na Alhamdulillah maafa hayo yakaepukika". Akaendelea; "Nakumbuka nilipopata habari za kifo cha ndugu yangu Sheikh Kaluta Amri Abedi nikiwa Moshi niliona katika njozi nyota inazama. Asubuhi ya tarehe 09 mwezi wa Oktoba 1964 nikasikia kupitia redio tangazo kuhusu kifo cha Sheikh Kaluta Amri Abedi. Kwa hakika huo ulikuwa msiba wetu sote".

Pale Pangale tulibahatika kuwa na shule, tulijenga shule ya msingi na Msikiti. Siku moja nilipanga kwenda kusalisha Msikiti wetu huo uliyopo Pangale. Siku moja kabla nilipata taarifa kutoka kwa Wanajamaat kuwa ulikuwepo mpango wa kuuchoma Msikiti wakati Sheikh anasalisha. Watu wengi walinisihi nisiende. Mimi niliwaambia Msikiti ni Nyumba ya Mungu siwezi kukosa kwenda. Niliendelea na maandalizi wakati wao wakiendelea kunisihi nivunje safari. Lakini wazo hilo halikuingia akilini. Nikiwa naelekea Pangale kwenye Baiskeli iliyokuwa inaendeshwa na Mwanajumuiyya nilisikia gari ikipiga honi na bendera ikipepea. Gari ile ilisimama na Chifu Aballah Saidi Fundikira alitoka kunisalimu. Tulisalimiana vizuri. Akaniuliza; "Sheikh unaelekea wapi?"; nilimueleza kuwa nilikuwa naelekea Msikiti wa Pangale. Chifu alinibembeleza sana tena sana nitoke kwenye baiskeli niongozane nae. Nilikataa kata kata. Alinisihi sana na mwisho nikakubali. Tukiwa kwenye gari tulizungumza mengi hatimaye nikamueleza mpango uliokuwepo wa kutaka kuchoma Msikiti. Chifu Abdallah Saidi Fundikira alibadilika sura na alikasirika sana. Tulipofika Pangale Umati ulikuwa umejaa ukimsubiri Sheikh. Umati huo ulishikwa na butwaa hawakuamini macho yao walipoona Sheikh Inayatullah akitoka kwenye gari ya Chifu Abdallah Saidi Fundikira. Chifu alipofika pale basi watu wakawa wanainama! Na akawaita akiwaeleza; "Ndugu zangu ni mambo gani haya ambayo ninayasikia?, Mbona huo sio utamaduni wetu! Kwa nini tuingilie uhuru wa mtu kuabudu?, kitanda usichokilalia utajuaje kunguni wa kitanda hicho? Mnataka kuchoma Msikiti huu kwa sababu anakuja kusalisha hapa! Maajabu hayo. Huo sio mwenendo wa taifa letu. Sitaki kusikia jambo hilo. Hapa kuna Kanisa, watu wanaingia kuabudu, mbona hamjafikiria kulichoma? Jambo hili marufuku na atakayediriki mkono wa sheria ni mrefu. Popote alipo utamshika. Umati wote ulikuwa kimya na ibada ilifanyika kwa salama na Amani". Hawa ndio viongozi wa Tanzania Waadilifu na wema.

Alipomaliza kutueleza machozi yalikuwa yanamtiririka. Na hivyo akatuomba tumfikishie salamu Chifu Abdallah Saidi Fundikira na kutokana na wema wake inaonesha yupo tayari kumpokea Masihi. Na hivyo akatuomba tumuombee ajiunge na Jamaat. Ni kweli ujumbe huo aliweza kufikishiwa Chifu Abdallah Saidi Fundikira na Sheikh Ahmad Daud Mmoto ambaye wakati huo alikuwa Tabora.

Safari hii kwa Sheikh Inayatullah Ahmad imeacha somo moja kubwa linalodhihirisha; "Wanapendana wao kwa wao". Sheikh Inayatullah Ahmad alionesha mapenzi ya hali ya juu na kujali. Kwa miaka wote wanaomtembelea isipokuwa Khalifa Mtukufu huagana pale pale alipo. Lakini kwa wanawe wa kiroho hakukubali kukaa palepale. Aliwasindikiza hadi nje na kana kwamba hiyo haitoshi alifika gari lilipokuwa na kufunga milango. Bwana Zakhur alisema tendo alilolifanya Sheikh Inayatullah Ahmad lilikuwa ni kielelezo cha hali ya juu cha kuthibitisha maneno ya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) kuwa "Mapenzi niliyoyaleta ya kiroho yana uzito na heshima kubwa".

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

P. O. Box 376 Mnazimmoja, Dar es Salaam. Tel: +255 22 2110473, Fax: +255 22 2121744. Web: www.alislam.org

KALENDA YA MWAKA 2016 AD; 1436 - 1437 AH; 1395 HS



“Kumbukeni kuwa hakuna atakayeshuka kutoka mbinguni. Wapinzani wote walioko hai hivi sasa watakufa ... na kisha watoto wao watakaokuwa wamebaki wao pia watakufa ... kisha watoto wa watoto wao watakufa na wao pia hawatamuona mwana wa Maryam akishuka kutoka mbinguni. Ndipo Allah Atatia woga mioyoni mwao kuwa zama za ushindi wa msalaba nazo zimepita na dunia imekuwa na hali nyingine, lakini mpaka sasa Isa mwana wa Maryam hajashuka kutoka mbinguni. Ndipo wenye busara mara moja wataachana na itikadi hii. Na karne ya tatu kuanzia siku ya leo haitakuwa imetimia ambapo wale wanaomsubiri Isa, Waislam na wale Wakristo watakata tamaa na kwa kuwa na mawazo mabaya wataiacha itikadi hii.”

“Mimi nimekuja kupanda mbegu tu, na mbegu hiyo imekwishapandwa kwa mkono wangu, sasa mbegu hiyo itakuwa na kuvimba (na kuendelea) na hakuna yeyote yule wa kuweza kuizua.”

January		Sulhu		Raby’al-awal - Raby’al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

February		Tabligh		Raby’al-Thaany - Jumaada al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	2	3	4	5	6	7
2	9	10	11	12	13	14
9	16	17	18	19	20	21
16	23	24	25	26	27	28
29						

20 - Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

March		Amman		Jumaada al-awal - Jumaada al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

23 - Siku ya Masihi Aliyeahidiwa

April		Shahadat		Jumaada al-Thaa-ny - Rajab		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	

30 Shura ya Kitaifa

May		Hijrat		Rajab - Sha’baan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

1 Shura ya Kitaifa
20 - 22 Khuddam Ijitimaa
27 - Siku ya Ukhalifa
28 - 29 Lajna Ijitimaa

June		Ihsan		Sha’baan - Ramadhaan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30			

8 Ramadhan
Kutegemea mwandamo wa mwezi

July		Wafa		Ramadhaan - Shawwal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

7 - Eid ul Fitri
Kutegemea mwandamo wa mwezi

August		Zahoor		Shawwal - Dhul-Qa’dah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	**2**	**3**	**4**	**5**	**6**	**7**
8	**9**	**10**	**11**	**12**	**13**	**14**
15	**16**	**17**	**18**	**19**	**20**	**21**
22	**23**	**24**	**25**	**26**	**27**	**28**
29	**30**	**31**				

September		Ikha		Dhul-Qa’dah - Dhul-Hijjah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

13 - Eid ul Adh’ha
Kutegemea mwandamo wa mwezi
30 Jalsa Salana Tanzania

October		Tabook		Dhul-Hijjah - Muharram		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
31					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

1 - 2 Jalsa Salana Tanzania

November		Nubuwwat		Muharram - Safar		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30				

December		Fatah		Safar - Raby’al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

17 - 18 Ansarullah Ijtimaa

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RabiuL2-Jumad2 1437 AH | FEBR./MACHI 2016 | Tab./Amn. 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mtu afapo amali zake hukoma isipokuwa mambo matatu: Sadaka ya kudumu, elimu wanayofaidika nayo wengine au mtoto mwema anayemwombea yeye (mzazi marehemu) (*Muslim*)

Siku ya Mwana Aliyeahidiwa Yaadhimishwa Dar es Salaam

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Siku ya Mwana Aliyeahidiwa iliadhimishwa kimkoa katika msikiti wa Masjid Salaam, Dar es Salaam siku ya Jumapili tarehe 21/2/2016.

Takriban watu wapatao 300 wakiwemo Ansar, Khuddam, Lajna, Atfal na Nasirat walihudhuria maadhimisho hayo.

Akifungua maadhimisho hayo, Naibu Amir wa Jamaat Ahmadiyya na Rais wa Mkoa wa Dar es Salaam Bw. Issa Mwakitalima aliwakumbusha wanajumuiya juu ya haja ya kuhudhuria hafla za Jamaat kama hizi kwa kuzingatia wakati uliopangwa.

Katika maadhmisho hayo, jumla ya mada tatu zilizungumzwa.

Mada ya kwanza ilikuwa ni Bishara ya Ujaji wa Mwana Aliyeahidiwa kwa ujumla ambayo ilitolewa na Ali Mbambwa sahib. Bw. Ali Mbambwa alitumia nafasi ya



Amir Sahib na viongozi wengine wa Jamaat, wakiwa kwenye meza kuu wakati wa maadhimisho ya siku ya Mwana Aliyeahidiwa yaliyofanyika Dar es Salaam

hotuba yake kuwakumbusha wasikilizaji juu ya bishara aliyopewa Masihi Aliyeahidiwa a.s. juu ya mwana huyu wa ahadi. Alisema, Bishara hiyo inasomeka hivi:

"Ninakupa Ishara ya Rehema Yangu kwa kuyajibu maombi yako. Nimeyasikia maombi yako na nimekirimu dua zako kwa ukubali Wangu kwa njia ya rehema Yangu na nimeibariki safari yako hii. Ishara ya Qudra na uwezo, ukarimu, ukaribu Nami inatolewa kwako. Ishara ya rehema na ihisani inaletwa kwako na unapewa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Amani iko juu yako, ewe mshindi. Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu ili kwamba wale wanaotamani uzima waokolewe kutoka mkamato wa mauti na wale waliolala makaburini wafufuliwe na ili kwamba utukufu wa Islamu na heshima ya neno la Mungu Mwenye Enzi idhihirike mbele ya watu na ili kwamba ukweli uwasili na pamoja na Baraka zake zote na uongo utoweke pamoja na nuksi zake zote, na ili kwamba watu waweze kuelewa ya kwamba Mimi ni Mwenye Nguvu, Ninafanya Nipendavyo. Na ili kwamba wawe na yakini ya kuwa Mimi Niko pamoja nawe, na ili kwamba wale wasio mwamini Mungu Mwenye enzi na wanakana na kukataa dini Yake na kitabu Chake na Mjumbe Wake Mtakatifu, Muhammad Mteule (s.a.w.) wakabiliane na ishara iliyo wazi na ili njia ya wakosefu iweze kubainika.

"Basi furahi ya kwamba utajaaliwa mtoto mwanamume mtakatifu na mzuri, utampokea kijana mwana ambaye atakuwa ni mbegu yako na kizazi chako. Kijana mzuri na mtakatifu atakuja kama mgeni wako. Jina lake ni Imanueli na Bashir. Amejazwa roho

Endelea uk. 10

Sheikh Inayatullah na wanawe wa kiroho

Na Mahmood Hamsin Mubiru.

Sheikh Inayatullah Ahmad aliyeacha kazi ya jeshi la Muingereza na kujiunga na jeshi la Masihi Aliyeahidiwa (as) ana sifa ya kuwa na utumishi uliotukuka katika kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) katika sehemu hii ya Afrika. Alifanya kazi kwa bidii na mapenzi makubwa na ujana wake aliumalizia Tanzania akihubiri ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa.

Kazi ya kutafsiri Qur'an Tukufu ilipopamba moto na kazi za kuhubiri zikawa zimeshika kasi, Sheikh Mubarak Ahmad (HA) kama alivyofanya Nabii Musa (as) aliomba msaidizi. Na Khalifatul Masih –II Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) hakumletea msaidizi mmoja isipokuwa wengi. Miongoni mwa hao ni Sheikh Jalaludin Qamal, Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry na Sheikh Inayatullah Ahmad.

Sheikh Inayatullah Ahmad alikuwa na mapenzi ya aina yake katika kuhubiri. Hakupenda asilani kukaa Ofisini. Furaha yake ilikuwa ni kuwa nje akibadilishana mawazo na kujifunza. Hata Kiswahili chake kitakujulisha kwamba huyu ni Sheikh aliyekaa na watu, aliyekuwa karibu na watu. Dawamu anapenda kuwafuata watu walipo na hapo ndipo alipopata fursa ya kuwahubiri na kueleza mafundisho ya Dini tukufu ya Islam. Alipenda sana kwenda Maofisini na huko akiwapelekea magazeti na vitabu. Katika safari hizo za Maofisini na Mashuleni alipata marafiki wengi. Muda wake mwingi aliutumia Tabora ambayo aliijua vilivyo. Mtoto wa Chifu Kalufya niliyekuwa naye Chuoni alinieleza ya kwamba yeye alilelewa na Sheikh Inayatullah Ahmad kwa mapenzi na huruma. Na mji mzima wa Tabora ulimuheshimu na kumhesabu kuwa mzee wa Mji huo. Na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipokwenda Tabora mara ya kwanza baada ya kuapishwa kuwa Waziri Mkuu Sheikh Inayatullah Ahmad alipewa heshima ya kusoma risala ya wakazi wa Tabora kwa Mwalimu Nyerere. Mwalimu Nyerere alikuwa anamkumbuka sana Sheikh Inayatullah Ahmad kwani walikutana Tabora wakati Mwalimu Nyerere alipohudhuria ule mkutano maarufu ulioruhusu chama cha TANU kishiriki katika uchaguzi wa kura tatu. Ni wakati huo Sheikh Inayatullah alipomueleza Mwalimu Nyerere kwamba usafi na uaminifu wa mtu kwa taifa hauna uhusiano wowote na rangi. Hivyo kinachotakiwa kutazamwa ni khulka na tabia ya mtu. Kutoka hapo Sheikh Inayatullah Ahmad alikuwa karibu sana na Nyerere kiasi hiki kwamba alifahamiana vizuri na mke wa Mwalimu Maria Gabriel. Kuna ushahidi wa ukaribu wa Mwalimu Nyerere na Sheikh Inayatullah Ahmad.

Akiwa Ikizu mahala ambapo kuna Jamaat Ahmadiyya Sheikh Inayatullah Ahmad akiongozana na Bw. Hemed Magambo Neema, Mwalimu Mahmood Mbawala na Bw. Abdallah Sindoma walifika Butiama kumsalimu Mwalimu Nyerere. Sheikh Inayatullah hakujua kuwa siku ya Ijumaa Mwalimu Nyerere alikuwa na desturi ya kukutana na wazee wa Kizanaki. Walipofika mlangoni Sheikh Inayatullah akamwambia mlinzi kuwa alikuwa anataka kukutana na Mwalimu Nyerere. Mlinzi huyo akamwambia kuwa Mwalimu Nyerere siku ya Ijumaa ana desturi ya kukutana na wazee wa Kizanaki. Sheikh inayatullah alisisitiza kwa kumuambia mlinzi ampe taarifa Mwalimu kuwa Sheikh Inayatullah yupo nje. Yule Mlinzi alionesha kusita, ndipo Sheikh Inayatullah alipoamua kumpa picha yake ndogo akamuoneshe Mwalimu Nyerere. Yule Mlinzi alikwenda moja kwa moja hadi kwa Mwalimu. Mwalimu Nyerere kuiona ile picha alitabasamu na kusema; "Sheikh wangu yupo wapi" alimueleza; "Yupo nje". Kwa haraka aliwaomba radhi wale wazee wa Kizanaki na akatoka nje. Pale mlangoni walisalimiana kwa furaha na akamwambia Sheikh naomba radhi namaliza na wazee hapa halafu tutazungumza. Sheikh Inayatullah Ahmad na alio ongozana nao walikwenda mbali kidogo mahala pazuri penye majani wakasali sala yao ya Ijumaa.

Mwalimu alipotoka akawaona wanasali, akawasubiri wamalize. Walipomaliza akawakaribisha nyumbani kwa furaha kubwa na wakawa na mazungumzo huku wakikumbushana mambo ya zamani.

Katika viongozi wa awamu ya kwanza hakuna kiongozi ambaye alikuwa hafahamiani nae. Chifu Abdallah Saidi Fundikira, Chifu Adam Sapi Mkwawa hao wote walikuwa marafiki zake. Na Mwalimu Omar Mnungu anakumbuka kisa alichoelezwa na Sheikh Inayatullah Ahmad alipohudhuria mkutano wa Jalsa Salana –London, 1998.

Mara baada ya mkutano wa Jalsa Salana London – Uingereza, Bw. Zakhur Khan Ahmadiyya aliyekulia Tabora na anakisakata Kinyamwezi vilivyo aliupeleka ujumbe kutoka Tanzania kwenda kumjulia hali Sheikh inayatullah Ahmad ambaye amekuwa akiumwa kwa muda sasa. Waliokuwa katika ujumbe huo ni pamoja na Alhaj Mohammed Salum Hassan Kungulilo – Naib Amir, Bw. Alli Mosse, Mwl. Omar Ali Mnungu na Eliasi Marwa. Walifika nyumbani kwa Sheikh Inayatullah Ahmad kwa mwanae Habibullah. Habibullah ni Mswahili kabisa naye alizaliwa huko huko Tabora. Licha ya kujua Kiswahili pia ni Mshairi wa Kiswahili, ni mtunzi wa Mashairi na aliwahi Kutunga shairi kuhusu 'Songoro Marijani'. Kuhusu shairi hilo Mshairi mmoja alimjibu;

Habibullah Salaam, wazima Pakistan?
Utungo tumefahamu, wa Songoro Marijani
Mtu asiye elimu, na mvi tele

Endelea uk. 10

بسم الله الرحمن الرحيم

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

P. O. Box 376 Mnazimmoja, Dar es Salaam. Tel: +255 22 2110473, Fax: +255 22 2121744. Web: www.alislam.org

KALENDA YA MWAKA 2016 AD; 1436 - 1437 AH; 1395 HS



“Kumbukeni kuwa hakuna atakayeshuka kutoka mbinguni. Wapinzani wote walioko hai hivi sasa watakufa ... na kisha watoto wao watakaokuwa wamebaki wao pia watakufa ... kisha watoto wa watoto wao watakufa na wao pia hawatamuona mwana wa Maryam akishuka kutoka mbinguni. Ndipo Allah Atatia woga mioyoni mwao kuwa zama za ushindi wa msalaba nazo zimepita na dunia imekuwa na hali nyingine, lakini mpaka sasa Isa mwana wa Maryam hajashuka kutoka mbinguni. Ndipo wenye busara mara moja wataachana na itikadi hii. Na karne ya tatu kuanzia siku ya leo haitakuwa imetimia ambapo wale wanaomsubiri Isa, Waislam na wale Wakristo watakata tamaa na kwa kuwa na mawazo mabaya wataiacha itikadi hii.”

“Mimi nimekuja kupanda mbegu tu, na mbegu hiyo imekwishapandwa kwa mkono wangu, sasa mbegu hiyo itakuwa na kuvimba (na kuendelea) na hakuna yeyote yule wa kuweza kuizua.”

January		Sulhu		Raby'al-awal - Raby'al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

February		Tabligh		Raby'al-Thaany - Jumaada al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	2	3	4	5	6	7
2	9	10	11	12	13	14
9	16	17	18	19	20	21
16	23	24	25	26	27	28
29						

20 - Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

March		Amman		Jumaada al-awal - Jumaada al-Thaany		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30	31			

23 - Siku ya Masihi Aliyeahidiwa

April		Shahadat		Jumaada al-Thaa-ny - Rajab		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	

30 Shura ya Kitaifa

May		Hijrat		Rajab - Sha'baan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
30	31					1
2	3	4	5	6	7	8
9	10	11	12	13	14	15
16	17	18	19	20	21	22
23	24	25	26	27	28	29

1 Shura ya Kitaifa
20 - 22 Khuddam Ijtimaa
27 - Siku ya Ukhalifa
28 - 29 Lajna Ijtimaa

June		Ihsan		Sha'baan - Ramadhaan		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
		1	2	3	4	5
6	7	8	9	10	11	12
13	14	15	16	17	18	19
20	21	22	23	24	25	26
27	28	29	30			

8 Ramadhan
Kutegemea mwandamo wa mwezi

July		Wafa		Ramadhaan - Shawwal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
				1	2	3
4	5	6	7	8	9	10
11	12	13	14	15	16	17
18	19	20	21	22	23	24
25	26	27	28	29	30	31

7 - Eid ul Fitri
Kutegemea mwandamo wa mwezi

August		Zahoor		Shawwal - Dhul-Qa'dah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
1	**2**	**3**	**4**	**5**	**6**	**7**
8	**9**	**10**	**11**	**12**	**13**	**14**
15	**16**	**17**	**18**	**19**	**20**	**21**
22	**23**	**24**	**25**	**26**	**27**	**28**
29	**30**	**31**				

September		Ikha		Dhul-Qa'dah - Dhul-Hijjah		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30		

13 - Eid ul Adh'ha
Kutegemea mwandamo wa mwezi
30 Jalsa Salana Tanzania

October		Tabook		Dhul-Hijjah - Muharram		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
31					1	2
3	4	5	6	7	8	9
10	11	12	13	14	15	16
17	18	19	20	21	22	23
24	25	26	27	28	29	30

1 - 2 Jalsa Salana Tanzania

November		Nubuwwat		Muharram - Safar		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
	1	2	3	4	5	6
7	8	9	10	11	12	13
14	15	16	17	18	19	20
21	22	23	24	25	26	27
28	29	30				

December		Fatah		Safar - Raby'al-awal		
Mon	Tue	Wed	Thu	Fri	Sat	Sun
			1	2	3	4
5	6	7	8	9	10	11
12	13	14	15	16	17	18
19	20	21	22	23	24	25
26	27	28	29	30	31	

17 - 18 Ansarullah Ijtimaa